# Nipashe

Jumamosi Aprili 20, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581652

www.ippmedia.com MWANGA WA JA...

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ

LIKE & FOLLOW US




UK.4

**DED** anayedaiwa kubaka mfanyakazi wa ndani, mbaroni

UKURASA 5

**OSHA** kuwanasa wenye kampuni zisizosajiliwa



UKURASA 7

**Majaliwa** ataka CAG apewe uhuru



**ARTETA: TUTASAJILI MSHAMBULIAJI MPYA**

UKURASA 21



# Warioba: Mtazamo wa nchi mbili hatari kwa Muungano

• **Anyooshea** kidole mambo ya kumulikwa...*Uk. 2*

## Tanzania, Uturuki zatia saini hati 6 makubaliano

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan wakishuhudia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba (kushoto) na Rais wa Baraza la Elimu Uturuki, Prof. Erol Ozvar wakitia saini makubaliano ya ushirikiano katika nyanja ya elimu ya juu baina ya nchi hizo mbili, jijini Ankara juzi. **PICHA: IKULU**

## Miradi, taasisi 180 yachunguzwa

UK. 2





MIAKA 60 YA MUUNGANO

OFA KATIKA TOLEO MAALUM!!

Katika kuadhimisha Siku ya Muungano mwaka huu, tarehe 26 April 2024 Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian Itatoa toleo maalum la Muungano, hivyo inawakaribisha kutoa salamu za kumbukizi, matangazo, picha na makala za mafanikio katika kusherekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa PUNGUZO MAALUM

Wahi mapema kwa sikukuu hii upate PUNGUZO, Artwork ya bure na nafasi katika majukwaa yetu ya kidigitali.

*vigezo na masharti kuzingatiwa*

The Guardian Nipashe

KWA MAWASILIANO TUPIGIE | +255 677 020 701

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz Au Tutembelee The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Mkabala na ITV / Radio One, Dar es Salaam
Tovuti: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com



**MICHEZO** SIMBA, YANGA NA SAFARI YA UBINGWA UK.24

**MAONI,** UK.6



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ya wizara hiyo, Bungeni jijini Dodoma jana, ambapo ameomba Sh. trilioni 1.1. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Warioba: Mtazamo wa nchi mbili hatari kwa Muungano

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, ametaka Muungano ujikite kuimarisha maisha ya wananchi na viongozi wazungumzie Tanzania zaidi badala ya kuigawa.

Aidha, zishirikiane katika masuala ya kisera hasa katika uchumi hata kama jambo hilo halipo katika Muungano.

Katika mahojiano maalum yaliyofanyika jana nyumbani kwake jijini Dar es Salaam kuhusu miaka 60 ya Muungano ambayo kila mwaka huadhimishwa Aprili 26, Warioba alisema suala ambalo wananchi wanaweza kulizungumzia ni kuhusu muundo wa serikali na kuwataka ifike mahali waamue.

"Miaka 30 tunazungumzia hili, linatupotezea wakati, badala kuzungumzia maendeleo tunazungumzia siasa za serikali," alionya.

Alisema, wanakoelekea ni kuimarisha huduma kwa mwananchi jambo litakaloleta umoja zaidi, mshikamano na kulinda amani ya nchi.

Alisema Muungano umesaidia katika umoja na amani, na kwamba jambo la msingi ni kuimarisha maisha ya wananchi.

Alikumbusha kuwa miaka mingi kumeonekana wanazungumzia siasa zaidi na changamoto zinazohusu madaraka.

"Tunapoteza muda mrefu kuzungumzia kuhusu madaraka. Tunapokwenda tunajenga nchi moja hata ukienda katika nchi ambazo zina muungano hawahangaiki kuzungumzia madaraka ya huyu ama yule, nenda India, yale majimbo yana madaraka, lakini wanaangalia maslahi ya India.

"Ni kweli hata viongozi wameendelea kuwa na lugha ya pande mbili. Ninataka tufike mahali tuzungumzie Tanzania, hata siku hizi kuna viongozi unaona mazungumzo yao wanasema serikali ya Bara, sio serikali ya Muungano, anataka serikali ya Bara tena pande zote ni kama wanataka tusiungane," alisema.

Alionya kuwa kugawanya madaraka kwa kuangalia hilo haliwezi kwenda katika Muungano na kero zote zinazozungumzwa zinahusu madaraka.

"Ninasema hivi tuangalie kero za wananchi, hayo mambo mengine hata hizo kero ukiwauliza wananchi, je, wanazijua watasema, hawazijui," alisema.

Alitaka watoke katika kuzungumzia madaraka waimarishe zaidi uhusiano na wananchi ili kupata maendeleo na kuachana na matatizo ya kiserikali na kurudi kwao.

"Tunaposema wamefaidika na hiki mara hiki. Sasa ni kuimarisha katika Katiba zote mbili, Katiba ya Muungano na ya Zanzibar kwa mwananchi wa kawaida, yale mambo ya Muungano sio mwongozo wake, yeye (mwananchi) anaangalia haki yake ameipata ya maendeleo," alisema.

Alisema kipindi kijacho kiwe ni kuimarisha haki zao kwa kuwa, kuna mambo ambayo bado yapo tofauti na ni lazima kuchukuliwe hatua hasa za kimaendeleo.

"Kwa mfano, huduma za afya kwa Mtanzania anataka apate huduma ya aina moja isije akawa anatoka Bara anahuduma ya aina hii, akitoka Zanzibar ana huduma nyingine.

"Kwa maana hiyo, kama kuna mpango wa bima iwe ni ya nchi nzima isije ukawa na bima Bara, ukienda Zanzibar haitumiki au ukiwa na bima Zanzibar, ukija Bara haitumiki ninadhani mambo kama haya tuyaimarishe iwe kwa Watanzania wote," alishauri.

Katika masuala ya mipango ya kiuchumi, alisema serikali zinatakiwa kushirikiana na yapo mambo mengi ambayo hawawezi kuyaachia kila upande kuandaa sera zake ama mipango yake, lazima kuyatekeleza kwa ushirikiano.

"Mfano uchumi wa buluu unategemea bahari, wanaoshughulika ni Watanzania kutoka pande zote kama unatengeneza sera ni lazima iwe sera moja ili wote waweze kuitumia.

"Mfano mwingine, utalii ni vizuri wakashirikiana wanaotoka nje wanaweza kwenda pande zote kama kuna mtalii anataka kwenda mbugani washirikiane kwa pamoja, badala ya kila upande kuwa na sera yake, inaweza kuleta faida kubwa wanakuja kwa pamoja wanapanga kama wataanzia Serengeti, Ngorongoro na kumalizia Zanzibar, ama wakaanzia Zanzibar na kuja Ngorongoro, Serengeti na Sadaan," alisema.

"Sera tunazozitengeneza tusije tukaona kwa kuwa suala sio la kimuungano basi unalitengeneza kwa upande mmoja lazima washirikiane," alishauri.

Alisema unapokuwa hauna sera ya pamoja unaweza kukuta biashara inakuwa tofauti na mtu akitaka kuanzisha kiwanda Zanzibar sera zipo tofauti.

"Mfano ukienda Zanzibar ikifika wakati wa kupiga kura utakuta wanayo sheria ya inasema Mzanzibar Mkazi maana yake ili uwe na haki ya kupiga kura uwe umeishi pale kwa miaka mitatu hii inaweza kuleta matatizo kwa kuwa, unaweza kuishi Unguja ukahamia Pemba mwaka mmoja, unakuja uchaguzi sheria inaonyesha haujaishi miaka mitatu ni kama inawabagua," alisema.

Alisema serikali ya Zanzibar imefika wakati ione ni mabadiliko gani wanayotakiwa kuyafanya kwa kuwa hayo ndiyo mambo yanayowakera wananchi na yanatakiwa kushughulikiwa.

"Haya mengine kwa kweli bado ninasisitiza mwelekeo wetu uwe ni kuwaungamisha wananchi kwa kila kitu kokote anakoishi, anajua anaishi Tanzania, tuache hii lugha wakati wote kuonesha kuna Tanzania Bara ama Tanganyika na kuna Zanzibar," alionya.

Hata hivyo, alisema Muungano upo imara changamoto zilizojitokeza ni za kawaida na wananchi wanaupenda.

"Haya tunayosema ni changamoto za serikali zisije kutukatisha tamaa tulipofikia ni mahali pazuri, alisema.

# Miradi, taasisi 180 yachunguzwa

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SERIKALI imesema imeanza uchunguzi wa miradi ya maendeleo 179 yenye thamani ya Sh. bilioni 61.01 iliyobainika kuwa na kasoro mbalimbali katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo 1,086 yenye thamani ya Sh. bilioni 743.9 iliyofanyika kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akizungumza bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25, alisema hayo na kuomba kuidhinishiwa Sh. trilioni 1.10.

Kadhalika alisema, uchambuzi wa mifumo 446 umefanyika kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika maeneo ya huduma za jamii, fedha, majengo, utawala, usafirishaji, biashara, umeme, kilimo na misitu.

Alisema upungufu huo unaochunguzwa ulibuliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), katika mwendelezo wa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2024/25 kupitia Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma (PSC), wanatarajia kufanya ukaguzi wa kawaida katika Taasisi za Umma 180 na Ukaguzi Maalum katika Taasisi za Umma 10 kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa rasilimaliwatu katika utumishi wa umma.

**UPATIKANAJI WATAALAMU UTUMISHI**

Simbachawene alisema katika mwaka 2024/25 ofisi hiyo itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuwezesha kupatikana wataalam katika Utumishi wa Umma maeneo ya vipaumbele ambayo ni pamoja na usimamizi michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika.

Vilevile, watumishi kupatiwa vitendea kazi, kuboresha maslahi na mafunzo ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya taasisi, kutoa taarifa na elimu kwa umma ili kukuza uelewa wa shughuli zinazotekelezwa na sekretarieti hiyo.

Wataimarisha utendaji kazi wa Taasisi kwa kutumia TEHAMA, kuimarisha upatikanaji wa takwimu za ajira; na kuimarisha uwajibikaji na udhibiti wa matumizi ya fedha na shughuli nyingine za sekretarieti ya ajira kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

**UTEKELEZAJI PSC**

Simbachawene alisema katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) inatarajia kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo kufanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za umma 180 na ukaguzi maalum katika taasisi za umma 10 kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa rasilimaliwatu katika utumishi wa umma.

Pia, atafanya mikutano minne kujadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, taarifa za masuala ya kiutumishi na kuhuisha miongozo ya Tume ya Uzingatiaji wa masuala ya Kiutumishi; kuelimisha wadau 1,500 katika Taasisi za Umma na Serikali za Mitaa kuhusu majukumuya Tume na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma na kuwajengea uwezo watumiaji 1,300 wa Mfumo mpya wa kielektroniki wa kushughulikia rufani.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wapili kushoto), akimsikiliza Mkurungenzi wa Teknolojia wa nishati jadidifu Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Adrera Mwijage (kulia), kuhusu majiko banifu ambayo yanatumia umeme kidogo na mkaa kidogo, kabla ya kufunga maonyesho ya nishati yaliyoandaliwa na Wizara ya Nishati katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. Wengine ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto) na (watatu kushoto) ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tanzania, Uturuki zatia saini hati za makubaliano

**Na Romana Mallya**

TANZANIA na Uturuki zimetia saini hati sita za makubaliano (MOU) zenye lengo la kuimarisha zaidi uhusiano baina ya nchi hizo mbili katika sekta mbalimbali za kimkakati kwa maendeleo ya pande zote mbili.

Makubaliano hayo yalishuhudiwa juzi na Rais Samia Suluhu Hassan na mwenyeji wake, Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, katika hafla maalum iliyofanyika katika ukumbi wa Rais nchini humo.

Hati za makubaliano zimejikita katika maeneo ya elimu, diplomasia ya uchumi na ushirikiano wa kitamaduni.

Kabla ya mapokezi rasmi ya serikali yaliyofanyika Aprili 18, Rais Samia alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Uzamivu katika Uchumi na Chuo Kikuu cha Ankara.

Wakati wa mkutano wa pamoja na waandishi wa habari, Rais Samia alielezea nchi hiyo kama 'mshirika wa thamani wa Tanzania' na Rais Erdogan alisema, Tanzania ni mojawapo ya 'washirika muhimu zaidi katika Afrika Mashariki'.

"Tumekubaliana mawaziri wetu na timu ya wataalamu wakutane na kuja na mfumo ambao unaweza kutumika kuweka mikakati ya utekelezaji wa eneo lililokubaliwa la ushirikiano," alisema Rais Samia wakati wa mkutano huo.

Marais hao wawili pia, walikuwa na muda wa kujadili mzozo unaoendelea Gaza, na Rais Samia alipongeza na kuunga mkono jukumu la Uturuki katika kutafuta suluhu la amani la mzozo wa kimataifa.

"Tunarudia wito wetu wa kusitishwa mara moja kwa uhasama huko Palestina na kuzuia ufikiaji wa kibinadamu kwa watu wa Gaza," alisema Rais Samia.

Rais Erdoğan alisisitiza haja ya kuongeza juhudi kukomesha mauaji hayo, usitishaji mapigano na muafaka wa kudumu kufikiwa haraka iwezekanavyo na lazima kuchukua hatua za kufikia suluhisho.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Rais Samia alisema ziara hiyo ni mwendelezo wa mageuzi katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje kupitia Diplomasia Uchumi.

"Thamani ya biashara baina ya nchi zetu imekua kutoka Dola milioni 11 mwaka 2003 hadi takribani Dola milioni 350 hivi sasa, ikichangia katika ajira, miundombinu, afya, viwanda na elimu ya juu.

Rais Samia alisema katika mazungumzo yao pia, walijadili suala la ulinzi na usalama ikiwamo kupambana na ugaidi na ushirikiano baina ya nchi hizo mbili katika eneo hilo.

Kadhalika, alisema wamegusia nafasi ya Uturuki kama mwanachama wa G20 katika kuunga mkono ajenda za nchi za Afrika katika majukwaa ya kimataifa.

Jana, Rais Samia alishiriki katika Kongamano la Biashara la Uturuki-Tanzania mjini Istanbul ili kushawishi wafanyabiashara wengi zaidi wa Uturuki kuja kuwekeza nchini Tanzania.

Takwimu zinaonesha thamani ya mauzo ya bidhaa za Uturuki kwa Tanzania imepanda kutoka Dola milioni 144 mwaka 2013 hadi Dola milioni 253 mwaka 2021, na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa waagizaji 11 bora, huku bidhaa za Tanzania zinazouzwa Uturuki zikiendelea kuwa ndogo kwa takriban Dola milioni 15 kwa mwaka.

Rais Samia yuko Uturuki kwa ziara rasmi baada ya kupata mwaliko wa Rais Erdogan, iliyoanza Aprili 17 na kukami-

# Makamu wa Pili ataka wananchi kutembelea maonyesho

**Na Restuta James**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ametoa rai kwa wananchi kutembelea maonyesho ya taasisi za Muungano yanayoangazia miaka 60 tangu Zanzibar na Tanganyika zilipoungana, ili kufahamu huduma na kutoa maoni ya namna ya kuuimarisha.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizindua maonyesho ya miaka 60 ya Muungano katika viwanja vya Mnazi Mmoja, yanayoshirikisha taasisi za muungano pamoja na wafanyabiashara wadogo.

Alisema katika maonyesho hayo, wananchi watapata fursa ya kufahamu huduma zinazotolewa na Taasisi za Muungano, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 na watapata nafasi ya kutoa maoni na ushauri utakaowezesha kuimarisha na kuudumisha.

"Muungano Wetu unatimiza miaka 60 ambapo tumeshuhudia mafanikio makubwa katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano, wameendelea kunufaika kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...umekuwa nyenzo na utambulisho muhimu wa umoja wetu," alisema.

Alisema katika miaka 60 iliyopita, serikali za pande zote zimesimamia utekelezaji wa masuala ya Muungano kwa ufanisi mkubwa ambao umefanikisha kuimarisha kwa utaifa, umoja, amani, utulivu na hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi.

"Kuwapo kwa Muungano kumesaidia sana kuimarisha hali za wananchi na kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano. Hali hiyo imetokana na kuwepo kwa soko la pamoja lisilokuwa na vikwazo vya kiutawala na kiuendeshaji linalojumuisha ushirikiano na utengamano unaorahisisha mtiririko wa rasilimali na bidhaa, mitaji, watu na huduma baina ya Tanzania Bara na Zanzibar," alisema Makamu huyo wa Pili, Abdulla.

Alisema Muungano umeibua fursa nyingi za kibiashara katika sekta za viwanda, hoteli na kujenga nyumba za biashara na makazi ambazo zimeongeza ajira kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Akizungumzia huduma za kijamii, alisema zimeimarika hususani za afya, maji, elimu, ustawi na maendeleo ya jamii na makazi na kwamba udugu wa damu umeimarika kwa kuwa wananchi wa pande zote za Muungano wameungana katika misingi ya ndoa na urafiki. "Taasisi 33 zimefungua Ofisi Zanzibar kati ya Taasisi 39 za Muungano. Hii ni hatua kubwa katika kuimarisha huduma kwa wananchi wetu na kuimarisha Muungano. Natoa wito kwa zile ambazo bado hazijafungua Ofisi Zanzibar kufanya hivyo," alisema.

Alisema ni wajibu wa kila Mtanzania kuulinda, kuuimarisha na kuudumisha akigusia kaulimbiu ya 'Tumeimarika na Tumeshikamana kwa Maendeleo ya Taifa Letu.'

Awali, Naibu Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, alisema maonyesho hayo ni mfululizo wa shughuli mbalimbali zinazoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kutoa elimu ya Muungano kwa makundi mbalimbali wakiwemo wananchi, wabunge, viongozi wa Serikali na wanafunzi.

# Majaliwa asema sasa nchi haina mgawo wa umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, serikali imetenga na kutumia zaidi ya Sh. trilioni 8.18 katika sekta ya nishati na kwamba kwa sasa nchini kuna uhakika wa umeme.

Aidha, ameagiza Wizara ya Nishati kusimamia kupunguza au kuondoa kabisa mrundikano wa maombi ya kuunganisha huduma za umeme na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), likomeshe ukiritimba na ucheleweshaji wa huduma hiyo.

Akifunga Maonesho ya Wiki ya Nishati yaliyofanyika viwanja vya Bunge, Majaliwa alisema sekta hiyo inagusa moja kwa moja maisha ya Watanzania na injini ya uchumi wa taifa ndiyo sababu ya Rais kuipa kipaumbele kwa kutenga fedha nyingi.

"Tunakumbuka miezi michache iliyopita tulikuwa na adha ya mgawo wa umeme hapa nchini. Jana nimemsikia Naibu Waziri Mkuu akitangaza kumalizika kwa mgawo wa umeme kwa nchi nzima. Ninampongeza sana kwa hatua hiyo muhimu. Ninatambua kazi kubwa aliyoifanya ili kuhakikisha utatuzi wa changamoto za upatikanaji wa nishati.

"Niseme tu sasa sekta ya nishati imetulia na Watanzania wanaendelea kupata huduma inayostahili ili kuinua maendeleo na kipato chao," alisema.

Majaliwa alisema katika sekta ndogo ya umeme, malengo makuu ya serikali ni kuhakikisha uzalishaji wa umeme unafikia megawati 5,000 ifikapo mwaka 2025.

"Kama nilivyotangulia kusema, kazi hiyo inafanyika kwa vitendo ambapo utekelezaji wa miradi ya kuzalishaji umeme ya Bwawa la Julius Nyerere megawati 2,115, umeme jua wa Kishapu Shinyanga megawati 150, Kinyerezi I Extention megawati 185 pamoja na miradi mingine inayoendelea ni kielelezo tosha cha kufikia malengo hayo," alisema.

Majaliwa aliwashauri wabunge kufunga mfumo wa gesi katika magari yao ili kuwasaidia kupunguza gharama za mafuta.

Akizungumzia nishati safi, Waziri Mkuu alisema serikali imeandaa mkakati wa kusimamia nishati safi ya kupikia ambao unatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni unaolenga ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania waitumie ili kupunguza vifo takribani 33,000 na kuokoa takribani hekta 469,420 za misitu ifikapo 2030.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema, "watu waamini TANESCO ni wakati umeme sio waleta umeme, na kwamba serikali imedhamiria kuondoa mtazamo huo kwa Watanzania kwa kuimarisha utendaji kazi."

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alishauri serikali itengeneze gridi ya maji kama ilivyo gridi ya umeme ili kukusanya maji ambayo yanasababisha mafuriko maeneo mbalimbali na kuwa na uhakika wa huduma hiyo.

Awali, akitoa taarifa ya maonesho hayo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, alisema hoja zilizojitokeza ni za umeme, nishati jadidifu ambapo asilimia 42 zilihusu maunganisho ya umeme kwenye vitongoji huku asilimia 24 ni za mafuta na gesi.

# Mkurugenzi anayetuhumiwa kubaka ashikiliwa

**Na Julieth Mkireri**

JESHI Polisi mkoa wa kipolisi Rufiji, linamshikilia aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Kassim Ndumbo, kwa tuhuma za kumbaka msichana aliyekuwa akimsaidia kazi za nyumbani.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, mkoa wa kipolisi Rufiji, Protas Mutayoba, alisema Mkurugenzi huyo anashikiliwa katika Kituo cha Polisi Mafia kwa ajili ya mahojiano.

"Ni kweli tunamshikilia kwa mahojiano aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mafia, Kassim Seif Ndumbo baada tukio hili kuripotiwa na tumepokea malalamiko akituhumiwa kumbaka msichana ambaye ni msaidizi wa kazi za nyumbani kwake," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutayoba hatua za awali zilizochukuliwa na Jeshi hilo ni kufanya mahojiano na mtuhumiwa huyo pamoja na mke wake ambao walisema msichana huyo ana umri wa miaka 18.

Pia, alisema msichana huyo bado hajapatikana na amedaiwa yupo safarini wilayani Korogwe huku uchunguzi wa tuhuma hizo ukiendelea na ikithibitika mtuhumiwa kuhusika, hatua za kisheria zitachukuliwa.

Aprili 18, Rais Samia Suluhu Hassani alitengua uteuzi wa Mkurugenzi huyo.



Dereva wa bajaji akikwepa shimo lililopo katika barabara iendayo Malamba Mawili, eneo la Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa baadhi ya madereva, eneo hilo liliharibika zaidi ya miezi mitatu iliyopita bila ya kufanyiwa ukarabati. **PICHA SABATO KASIKA**

## Mbunge adai Dk. Salmin anaishi mazingira magumu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Baraza la Wawakilishi, Suleiman Haroub Suleiman amesema Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour Juma, nyumba yake inakabiliwa na mmonyoko wa udongo kutokana na kuwa karibu na bahari.

Akiuliza swali bungeni jana, Suleiman alisema kuna baadhi ya viongozi ambao walitumikia Serikali ya Tanzania akiwamo Dk. Salmin, ambaye anaishi katika mazingira magumu.

Alihoji kama serikali ipo tayari kushirikiana na viongozi wa kamati ya Baraza Kuu la Wawakilishi Zanzibar ili kutatua hali hiyo.

"Pia kuna baadhi ya maeneo yanahitaji kutunzwa, lakini hadi sasa yako katika hali hatarishi ikiwamo shule aliyosoma Karume," alisema.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo alisema ofisi yake inashirikiana vizuri na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar wanalichukua suala hilo ili kujadili namna ya kuboresha maeneo hayo.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwaenzi na kuwatunza waasisi wa Muungano.

Dk. Jafo alisema serikali imekuwa na utaratibu wa kuwatunza, kuzitembelea na kuzifariji familia za waasisi wa taifa kama njia mojawapo ya kutambua mchango wa waasisi wa Muungano.

Aidha, alisema serikali inaendelea kuhakikisha kuwa kila mwaka kumbukumbu za kifo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na maadhimisho ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zinafanyika.

# Wananchi wampokea Nchimbi na kilio migogoro ardhi

**Na Halfani Chusi,** MBARALI

WANANCHI wamempokea Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kilio cha migogoro ya ardhi wilayani Mbarali.

Katika mkutano wake eneo la Ubaruku, ikiwa ni ziara yake katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wananchi walipaza sauti kuhusu migogoro baina yao na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mkazi wa eneo hilo, Zaile Mwanda, alisema changamoto kubwa wilayani humo ni mgogoro wa ardhi na chanzo chake ni serikali kutumia kitu alichokiita ubabe kurasimisha maeneo ya wanachi kuwa hifadhi.

"Sisi ni wanadamu tunazaliana na tunaongezeka. Serikali inakata maeneo inasema ya hifadhi, kuna vijana wetu wanaosoma wakifeli mitihani wanarudi kulima, lakini serikali imechukua maeneo yote.

Mwananchi huyo alidai; "sasa hivi maliasili wanajipigia tu watu risasi, wanasema huyu amevamia, watu wanakufa ni hatari sana mheshimiwa. Leo Serikali ya CCM inasema sisi tumevamia hifadhi wakati tupo hapo tangu enzi za Mwalimu (Julius) Nyerere (Baba wa Taifa)," alisema.

Mkazi mwingine, Salumu Malenga, alidai kuwa serikali imeweka bikoni katika mashamba ya watu kinyume na mpaka.

"Wapo watu wanampotosha Rais Samia Suluhu Hassan kwamba ile ni ardhi oevu, hayo ndiyo maneno yao kila siku.

"Nimeongea haya baada ya wewe kuondoka tutaanza kutafutwa na askari wa Jeshi la Polisi kwa ajili nimeongea, alisema Malenga ambaye alimkabidhi Balozi Nchimbi nakala inayojumisha malalamiko yao yote ya ardhi na mgogoro wao wa ardhi uliodumu kwa muda mrefu, ambapo Nchimbi alimtoa hofu mwananchi huyo kuwa hakuna atakayemkamata.

Magreth Mwakipesilie alizungumzia kitendo cha baadhi ya askari wa wanyama pori kuwaua kwa risasi watoto wao wanapokwenda kuvua samaki kwa ajili ya kutafuta riziki.

"Kama wao wanaona hawa watoto wameingia eneo isivyo sahihi, kwanini wasiombe serikali ikatenga eneo rafiki kwa ajili ya wavuvi. Wakiona mtu anakwenda kuvua badala ya kumpa elimu wanamchoma moto wanamuua," alidai na kuongeza:

"Kwa sisi tunaotunza watoto tumboni (mama) tunaumia sana tunamuomba Rais Samia atusaidie tupate ardhi yetu ili tuweze kulima na kupata kipato cha kulisha familia zetu. "Tunakuomba utufikishie kilio hicho kwa Rais Samia, atusaidie kwa sababu na yeye ni mzazi na amepitia uchungu wa kuzaa," aliomba.

Naye, Atela Kulubayi, alisema; "Kumekuwa na mgogoro mkubwa kwa suala la kilimo kupewa kipaumbele kuliko ufugaji, wafugaji tunaonekana hatuna maana kabisa, lakini ninaomba niulize utapewa wali bila mboga?"

"Hawataki mifugo wakati hata Yesu alizaliwa kwenye zizi la ng'ombe, wafugaji inapotokea wamekosa wawajibishwe kama watu wengine kwa mujibu wa sheria na sio mifugo yao kuuzwa," aliomba.

Akitoa ufafanuzi kuhusu utata wa mpaka kati ya hifadhi na wanakijiji, Balozi Nchimbi alisema atatoa maelezo kwa serikali kujiridhisha na utata huo na wataalamu watapita kutafuta.

Kuhusu manyanyaso ya wananchi dhidi ya askati wanyamapori, Balozi Nchimbi alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homela, kuhakikisha elimu inatolewa na kuonya askari wanaotumia nguvu zinazotweza utu.

Alivitaka vyombo vya serikali visimamie kuhakikisha matukio ya ukatili hayafanyiki dhidi ya raia. Kadhalika, aliagiza uongozi wilayani humo kuangalia namna nzuri ya kufanya watu wanaokwenda kuvua samaki wasipigwe.

Pia, alimtaka Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aanze mazungumzo na mmiliki wa Mbarali Estate, ili aachie moja ya mashamba yake kwa ajili ya wananchi.

Akifafanua kuhusu tozo ya ushuru wa Sh. 3,000, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbarali, Misana Kwangu, alisema ushuru wa mazao upo kwa mujibu wa sheria na mkulima anaposafirisha mzigo chini ya tani moja hatakiwi kulipia.

# OSHA kuwanasa wenye kampuni zisizosajiliwa

Na Elizabeth Zaya

WAKALA wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), imeanza kampeni ya kubaini kampuni, taasisi na ofisi zinazoendesha shughuli zake bila kusajili mahala zinapofanyika shughuli zake. Kaimu Meneja wa Masoko na Uhamasishaji, Shabani Mmbaga, alisema hayo wakati akizungumza katika semina ya Wahariri wa vyombo vya habari iliyoandaliwa na wakala huyo.

"OSHA tunasema unatakiwa kusajili eneo lako la kazi ili ikusaidie kukabili athari ambazo zinaweza kujitokeza katika eneo la kazi, kwahiyo tumeanza kampeni ya kupita kwenye maeneo yote ya kazi ambayo hayajasajiliwa, unaposajili eneo lako la kazi linakuwa salama," alisema Mmbaga.

"Waajiri wote ambao wana maeneo ya kazi na hawajasajili, na ieleweke kwamba usajili wa eneo la kazi ni jambo la kisheria na inazungumza wazi kwamba kila eneo la kazi lazima lisajiliwe na hakuna gharama."

Alisema kutokusajili eneo la kazi ni uvunjaji wa sheria na kwa mwajiri atakayebainika kukiuka atakumbana na mkono wa sheria.

"Unaposajili eneo lako la kazi sio tu unaepuka adhabu, lakini inakusaidia kupata faida ya huduma zinazotolewa na OSHA na kipindi hiki tunaelekea katika maadhimisho ya siku ya afya na usalama mahala pa kazi duniani, kwa hiyo ni vema tukasajili na kuokoa au kuwasaidia wale wanaofanya kazi katika taasisi au ofisi zetu," alisema Mmbaga.

Alisema sheria inatambua eneo la kazi ni lile ambalo mtu anafanya kazi kwa ajili ya kujipatia kipato.

"Unapokuwa unafanya shughuli yako yoyote ile ambayo unapata kipato, hakikisha eneo hilo linasajiliwa na kimsingi kuna maeneo makubwa ya kati na madogo, yote haya yana utaratibu wake wa kusajiliwa, tafadhali sana tunaomba hasa kwa yale maeneo ambayo ni rasmi angalau kwa kuanzia yasajiliwe ili iwe rahisi kupata huduma zetu ikiwa ni pamoja na kukaguliwa, kufanyiwa vipimo vya afya kwa wafanyakazi na kupata ushauri wa afya na usalama mahali pa kazi," alisema Mmbaga. Alisema sheria inaelekeza miongoni mwa adhabu kwa asiyesajili eneo la kazi ni pamoja na faini au kifungo na zote hizo zinatolewa kulingana na mazingira.

Sheria ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi Na.5 ya mwaka 2003, inaeleza kwamba msingi mkuu wa sheria hiyo ni kuwalinda na kuwaweka salama wafanyakazi katika mazingira ya kazi, kuwalinda dhidi ya vihatarishi wanapokuwa kazini.

Kadhalika, inamtaka mwajiri kupima afya ya mfanyakazi wakati anaajiriwa, akiwa kazini na baada ili imsaidie kupata haki zake hasa anapopata athari za kiafya kazini ambazo hakuwa nazo wakati anaingia.

Sheria hiyo pia, inaweka wajibu wa Mwajiri, kuhakikisha kwamba afya na ustawi wa mfanyakazi kazini unafanyiwa urekebu, yaani anapopata changamoto ya afya kazini ikiwamo kuugua na nyinginezo, kuhakikisha afya yake inaimarika na siyo kumfukuza kazi

Mfanyakazi, sheria hiyo ya inampa wajibu wa kutofanya mambo yanayoweza kuhatarisha afya na uslama wake au wa wafanyakazi wengine eneo la kazi.



Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Maximilian Chuhula (kushoto), akizungumza wakati wa uzinduzi wa kitabu kinachoelezea changamoto na matarajio ya utangamano wa Afrika na mgogoro wa Sahara, uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Katoliki Ruaha (RUCU), mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Awataka wasomi kutoogopa kufanya utafiti nje ya nchi

Na Francis Godwin, IRINGA

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk Maxmilian Chuhula, amewataka wasomi wa vyuo vikuu kutoogopa kufanya utafiti nje ya nchi ili wazijue tabia za watu wengine kwenye mataifa yao.

Dk. Chuhula ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Historia Tanzania, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa kitabu kinachohusu matarajio ya utengamo wa Afrika, mgogoro wa Sahara, mjini hapa.

Kitabu hicho kilicho chapishwa na Africa Proper Education Network (APE), kimeandikwa na Dk Maxmilian akishirikiana na mhadhiri mwingine wa UDSM, James Zotto.

"Fanyeni utafiti nje ya Tanzania mjifunze vitu vingi, mjifunze kuhusu watu wengine wa Afrika na muongeze maarifa," alisema na kuongeza;

"Kitabu hiki kina uhalisia na naamini mkikisoma kitawaongezea maarifa ya kutosha kuhusu utengamano wa Afrika hasa mgogoro wa Sahara Magharibi," alisema.

Pia, kitakuwa miongoni mwa vitabu vitakavyo wapatia wanafunzi uelewa kuhusu masuala ya utengamano wa Afrika, hasa mgogoro wa Sahara Magharibi.

Awali Zotto alisema uzinduzi wa kitabu hicho pia unamuenzi Profesa Gaudence Mpangala, aliyekuwa kati ya wasomi, wachambuzi mahiri kwenye masuala ya kisiasa, akifundisha RUCU mpaka mauti ilipomfika Februari 4, 2021.

"Profesa Mpangala ni kati ya wahadhiri waliomjenga kitaaluma hasa katika masuala ya historia na migogoro, alinisimamia na kumuenzi, tukaona tuje kuzindulia kitabu kwenye chuo hiki," alisema Zotto.

Mwandishi mwingine wa kitabu hicho, Dk. Chuhula ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Historia Tanzania amesema hakuna ubishi kwamba ili kuandika vitabu wanafunzi lazima wajikite katika kufanya utafiti.

Awali, Kaimu Mkuu RUDU, DK Makungu Bulayi, aliwataka wanafunzi kujenga tabia ya kusoma vitabu na kujikita katika uandishi ili kufikia malengo yao kitaaluma.

Alisema uzinduzi wa kitabu hicho umekiheshimisha chuo chao hasa wakati huu wa utandawazi ambao wanafunzi wanapaswa kujifunza mambo mengi zaidi kwa kusoma vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni tofauti.

Baadhi ya wanafunzi wa RUCU, walisema ujio wa kitabu hicho chuoni kwao utawapa mwanga mpana hasa wale waliojikita kwenye masuala ya historia. "Tumepata mwanga mkubwa sana kwa ujio wa kitabu hiki zaidi, tumejifunza kwamba tunaweza kufanya utafiti hata nje ya Tanzania," alisema Daud Daud, mwanafunzi wa RUCU.

# Sekondari Ngara kupendekezwa kuwa chuo kikuu

Na Judith Julius, NGARA

MWENYEKITI wa Bodi ya Shule ya Sekondari ya Ngara ya Wavulana, Mchungaji Aron Nkwale, amesema kuwa bodi itapendekeza shule hiyo ifanywe chuo kikuu.

Nkwale alisema hayo katika sherehe ya mahafali ya kidato cha sita iliyofanyika shuleni hapo juzi.

Alisema bodi ina mpango huo baada ya kuona hakuna shule yenye miundombinu bora wilaya nzima ya Ngara na kuongeza kuwa wanawashukuru waliopeleka huduma ya umeme.

Katika risala iliyosomwa na wahitimu mbele ya mgeni rasmi Nicholaus Jovin waliishukuru serikali kwa kujenga na kuboresha miundombinu katika shule yao na kuifanya kuwa ya kisasa. Walimweleza mgeni rasmi ufaulu kwa alama nzuri zaidi utaendelea katika shule hiyo.

Kwa mujibu wa wahitimu hao, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa mabweni, vyumba vya madarasa 12, matundu ya vyoo 15, jengo la utawala, bwalo, na upatikanaji wa umeme wa Tanesco kupitia mradi wa umeme, LADP2, unaoshirikisha nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi (NELSAP). Jitihada zote hizo zimefanyika chini ya uongozi wa wilaya.

Mafanikio mengine ni uongozi wa shule kushirikiana na halmashauri na serikali kuu kuruhusu fedha zinazotumwa zinafanya kazi bila kupindishwa matumizi na maelekezo.

NELSAP, kupitia Benki ya Dunia (WB), vile vile iliruhusu fedha za miradi miwili ya umeme kupitia kampuni ya Kelvin Electrical Company Limited na majengo kupitia kampuni ya GESAP.

Pia, alimkabidhi Mkurugenzi Msaidizi wa shule hiyo, Ramadhani Rusule, fedha ya kununua mipira mitano ya miguu na kikapu, pamoja na nyavu.

Mgeni rasmi alisema kuwa shule hiyo imepata kipaumbele kutokana na eneo ilipojengwa, akibainisha kuwa eneo hilo lilikuwa ni mahususi kwa wakimbizi waliokuwa wakihudumiwa na Shirika la Kimataifa la UNHCR.

Wahitimu hao walijiunga Juni 13, 2022 wakiwa jumla ya 228 wa kidato cha tano kwa tahasusi mbili za HKL na HGL, huku shule ikiwa inaongozwa na Abel Eliabu na makamu wake Nuru Baraka.

Ilianzishwa kwa mpango wa halmashauri kupitia fursa ya makambi ya wakimbizi kutoka Burundi na mahafali ya tatu tangu kuanzishwa kwake yalifanyika Aprili 18 mwaka 2020 ikiwa na jumla ya wanafunzi 148 pamoja na walimu saba.

Ilianzishwa kwa lengo la kutoa elimu bora na yenye ufanisi kwa wanafunzi kama isemavyo kauli mbiu 'Elimu kwa Ufanisi', kutoa na kuendeleza nidhamu kwa wanafunzi ili kujenga utamaduni wa taifa.

Shule imepata mafanikio kitaaluma, mwaka 2022 kati ya idadi ya wanafunzi 115 ufaulu wao daraja la kwanza (wanafunzi 34), la pili (wanafunzi 76), na la tatu (wanafunzi watano).

Aidha, hakukuwa na daraja la nne au la sifuri. Mwaka 2023 idadi ya wahitimu ilikuwa 228 na ufaulu wao daraja la kwanza (wanafunzi 96), la pili (wanafunzi 98), la tatu (wanafunzi wanane). Hakukuwa na daraja la nne au sifuri.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga wakati sahihi wachezaji 'kujinadi' sokoni

**MECHI** yoyote ya watani wa jadi wa soka, Simba na Yanga, inayochezwa hapa nchini ni kubwa bila kujali aina ya mashindano ambayo timu hizo mbili zinachuana.

Leo kwa mara nyingine watani hao wanakutana, ni katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, itachezwa kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin, Dar es Salaam.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi, ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 55, wamecheza mechi 21 na watani zao, Simba wako katika nafasi ya tatu, wameshuka dimbani michezo 20.

Azam FC , mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2013/2014 maarufu 'Wauza Lambalamba' wao wapo katika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo, wamejikusanyia pointi 51 kibindoni, lakini wamecheza michezo 23.

JKT Tanzania ya Dar es Salaam, Mashujaa FC kutoka Kigoma, Tabora United ya mkoani Tabora na Mtibwa Sugar ya Manungu Turiani, Morogoro ziko katika hatari ya kushuka daraja, ziko mkiani kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 16 za mikoa mbalimbali.

Kama ambavyo bado mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo ziko wazi, kwa kila timu inayohitaji kutimiza malengo yake inatakiwa kushinda mechi zote zilioko mbele yake, pia katika vita ya kujinusuru na janga la kushuka daraja, lolote linaweza kutokea.

Huku mkiani ndio mambo hayatabiriki, tofauti ya pointi ni chache, hivyo timu hizo zinazoburuza mkia endapo 'zitapindua meza' na kupata matokeo chanya kwenye michezo yake iliyobakia, msimamo wa ligi unaweza kubadilika na wale walioamini wako mahali salama kibao kikawageukia.

Kwa maana nyingine muhimu, bado kila timu ina nafasi ya kupigania kufanya vyema kwa sababu mbali na kumaliza kwenye nafasi nzuri, itajihakikishia kupata kiasi kikubwa cha fedha zinazotolewa kama zawadi na wadhamini wenye haki ya kurusha matangazo ya televisheni.

Kuelekea mechi ya leo, ambayo ni dabi mojawapo inayozungumzwa hapa barani Afrika, matokeo yoyote ya ushindi yataifanya timu iliyovuna kujiimarisha kwenye mbio za kutwaa taji hilo kwa msimu wa mwaka 2023/2024.

Lakini kikubwa tunawakumbusha wachezaji kuupa umuhimu na heshima inayostahili mchezo huo. Wachezaji wanatakiwa kufahamu kupitia viwango watakavyovionyesha katika dabi hiyo, vitatoa mustakabali, hatima na thamani zao kuelekea msimu ujao.

Wachezaji watakaojituma na kusaidia timu zao kupata matokeo chanya, mbali na ahadi nono za fedha watakazopewa, lakini kwa kila mmoja atajitengenezea mazingira mazuri ya kuboreshwa kwa mkataba wake na wale walioko ukingoni, kufanya mazungumzo ya mkataba mpya wakiwa na nguvu.


Pia tunawakumbusha mechi ya dabi hufuatiliwa na makocha na mawakala wa ndani na nje ya Tanzania, hivyo watumie fursa hiyo vyema kujiweka sokoni na kwa wale ambao 'nyota' zao zitang'ara, klabu zao zitapokea ofa kwa ajili ya kuwasajili na maisha mapya ya soka yataanzia hapo.

Mbali na kuonyesha ufundi na mbinu, nidhamu ni jambo muhimu linalotakiwa kuonyeshwa kwa wachezaji wa timu zote mbili kwa sababu zitawaongezea nafasi ya kuitwa katika timu za taifa lakini pia ni darasa kwa wachezaji wenzao chipukizi ambao watafuatilia mechi hiyo.

Mashabiki pia wanatakiwa kufahamu mipaka yao, wasiturudishe nyuma katika zama za kurushia wachezaji au waamuzi chupa za maji pale ambao wanapokasirishwa na matokeo au uchezeshaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Mwamuzi Arajiga chezesha vyema kama 'dabi' iliyopita

Na Adam Fungamwango

**MWAMUZI** Ahmed Arajiga amechaguliwa tena kuchezesha mechi ya watani wa jadi, maarufu kama 'dabi' itakayochezwa leo, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuanzia saa 11:00 jioni.

Arajiga ndiye aliyechezesha mechi iliyopita ya Novemba 5, mwaka jana, iliyochezwa kwenye uwanja huo huo, wenyeji Simba wakipokea kipigo kitakatifu cha mabao 5-1.

Ameingia katika rekodi ya kuchezesha mechi mbili za Ligi Kuu za Simba na Yanga kwa msimu mmoja, mzunguko wa kwanza na wa pili, kitu ambacho ni aghalabu sana kutokea.

Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na Bodi yake ya Ligi (TPLB), imemwamini kwa mara nyingine tena Arajiga si kwa bahati mbaya.

Ni kwa sababu mechi iliyopita alichezesha kwa makini na uwezo wa hali ya juu kiasi pamoja na Simba kufungwa idadi kubwa ya mabao, hakuna mwanachama au shabiki yoyote wa timu hiyo aliyemlaumu mwamuzi.

Kila mmoja aliyekuwa uwanja na aliyekuwa akiangalia kwenye televisheni alilaumu kile ambacho aliamini kilisababisha bila kumtaja mwamuzi.

Ndiyo maana hadi leo, si wengi wanaojua katika mechi ile, ni Arajiga aliyechezesha.

Kama angechezesha vibaya, si asingepewa tu mechi hii, lakini hata jina lake lingekuwa midomoni mwa mashabiki mpaka dabi hii ya leo itakapochezwa.

Baada ya mechi ile, mashabiki na wanachama na Simba, wengine walilaumu viongozi, kuna waliolaumu wachezaji, na wapo waliomlaumu aliyekuwa Kocha Mkuu, Roberto Oliveira 'Robertinho', na ndiyo mechi ilisababisha atimuliwe.

Arajiga, alifanya mashabiki kuongea soka badala ya kumzungumzia mwamuzi. Wanachama na mashabiki wa Yanga waliondoka wakimsifia Kocha, Miguel Gamondi na wachezaji wao kwa soka safi waliloonyesha kiasi cha kuibuka na ushindi huo mnono.

Alichofanya mwamuzi siku ile aliacha soka lichezwe na matokeo yaamuliwe kwa uwezo na viwango vya wachezaji na si yeye kutumia nguvu kutaka kuibeba timu moja au 'kubalansi.'

Baadhi ya waamuzi wanaochezesha mechi hiyo wanaonekana kuingia na presha zaidi kuliko hata wachezaji wenyewe.

Inawezekana kwa sababu ya woga wa dabi, au tayari ana maelekezo ya nani anatakiwa kushinda kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo rushwa.

Matokeo yake kunakuwa na maamuzi ya ovyo kiasi mechi ikimalizika, mashabiki badala ya kuzungumzia mpira, kusifu mbinu za makocha na uwezo ulioonyeshwa na wachezaji, anazungumziwa mwamuzi na maamuzi yake yote uwanjani.

Hali hii ilikuwa ikisababisha baadhi ya dabi kutokuwa na mvuto, badala yake lawama na kelele kutoka kwa mashabiki, ingawa ni kweli wapo baadhi yao ambao wao timu ikifungwa hata kama ikipoteza kimpira, mwamuzi anahusika.

Ninachomshauri Arajiga kuchezesha kama alivyofanya mechi iliyopita, akiacha soka lichezwe na matokeo yajiamue yenyewe kwa timu itakayoizidi nyingine kwa kiwango, mfumo na uwezo wa wachezaji wake uwanjani.

'Akopi na kupesti' kile alichokifanya siku hiyo ili aendelee kujizoea sifa kwa sababu inawezekana kabisa hata msimu ujao akapewa tena dabi nyingine kwa mara ya tatu au ya nne kabisa.

Ajiondolee lawama na kuwa nyota wa mchezo badala ya wachezaji. Asiogope kufanya maamuzi magumu kama alivyofanya mechi iliyopita dakika ya 85 alipotoa penalti kwa Yanga, wakati tayari Simba ikiwa 'imeshaloa' mabao manne.

Inapohitajika kadi ya njano, nyekundu, itoke, asisubiri kusawazisha makosa, yaani mmoja anafanya anamezea, halafu mwingine anafanya baadaye anaacha na sababu aliacha ile ya kwanza, mechi itamshinda.

Nafikiri Arajiga ataendelea kuchezesha vyema ili kujijengea heshima, kupewa mechi mbili za dabi ndani ya msimu mmoja si kubahatisha, ni dhahiri 'wakubwa' wamemwamini, lakini pia ni kama mtego kwake.

HABARI KITAIFA



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana akizungumza na viongozi wa CCM katika kikao maalumu cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Musoma Mjini, mkoani Mara juzi, akiwa katika ziara ya kuimarisha chama mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa ataka CAG apewe uhuru

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kasim Majaliwa, amesema bila uhuru, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hawezi kutimiza ipasavyo wajibu wake wa kuhakikisha uwazi na uwajibikaji vinakuwapo katika matumizi ya fedha za serikali.

Amesema nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), zinapaswa kutambua maeneo yanayostahili kutiliwa mkazo baina ya serikali, Bunge, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Taasisi za Ukaguzi na Mabunge kwenye nchi za SADC (SADCOPAC).

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akifunga Mkutano wa Kujenga Uelewa wa Pamoja na Ufanyaji wa Kazi wa Taasisi za Ukaguzi na Mabunge kwenye nchi za SADC (SADCOPAC), uliofanyika Zanzibar.

Majaliwa alisema miongoni mwa maeneo hayo ni kuunga mkono uhuru wa Ofisi ya CAG.

"Bila uhuru, CAG hawezi kutimiza wajibu wake ipasavyo katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji wa fedha za serikali. Kwa hiyo, wadau wote wanawajibika kulinda uhuru huu kupitia hatua za kisheria na msaada wa taasisi zenu," alisema.

Alisema suala la kuimarisha uhusiano kati ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (AG) na Bunge ni la muhimu, kwa kuwa linasaidia kurahisisha utendaji kazi baina yao.

"Ushirikiano kati ya vyombo hivi unawezesha utendaji na usimamizi rahisi. Unaruhusu uchunguzi mzuri zaidi wa matumizi ya fedha za serikali. Ushirikiano huu unaweza pia kuboresha utawala na uwajibikaji ndani ya nchi wanachama," alisema.

Majaliwa aliwataka washiriki wa mkutano huo waweke kipaumbele kuboresha utawala bora na uwajibikaji kwenye nchi zao.

"Kupitia hatua za kisheria na usimamizi, tunapaswa tuhakikishe kuwa, mifumo iko sawa na inaweza kuziwajibisha taasisi za serikali kupitia matumizi yao. Kwa kuzingatia haya, tunaweza kukuza uaminifu katika mifumo yetu ya utawala na ustawi wa raia wetu," alisema.

Katika kusisitiza ushirikiano wa kikanda, Majaliwa aliwaambia washiriki wa mkutano huo kwamba, ushirikiano baina ya SADCOPAC na washirika wa kikanda unapaswa kuendelezwa na kuwaahidi kuwa, Tanzania ikiwamo Zanzibar zimejipanga kikamilifu kufanya kazi bega kwa bega na washirika hao ili kuboresha shughuli za ukaguzi kwenye ukanda huo.

Alisema serikali imejitolea kusaidia Taasisi Kuu za Ukaguzi (Supreme Audit Institutions), Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali (PACs) na wadau wengine muhimu ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora na ya uwazi ya rasilimali za umma, njia ambayo inakuza utawala bora.

Awali, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Mudrik Ramadhani Soraga, alisema Tanzania imefaidika kiuchumi na kimkakati kutokana na mkutano huo kufanyika nchini.

Alisema wabunge na wawakilishi waliokutana wamejadili mada ambazo zitawawezesha kusaidia serikali zao katika nchi za SADC kuimarisha uwajibikaji na matumizi mazuri ya rasilimali na mapambano dhidi ya rushwa.

"Lakini, nikiwa waziri mwenye dhamana ya utalii, mkutano huu umetuongezea mapato," alisema Soraga.


Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Dk. Othman Abbasi Ali, ambaye ofisi yake ilikuwa mwenyeji wa mkutano huo, alisema mbali na kuimarisha ushirikiano, mkutano huo umetoa fursa kwa wajumbe wa PAC katika mabunge kubadilishana uzoefu wa njia bora za kufuatilia matumizi bora ya fedha za serikali katika nchi zao.

Mbunge kutoka Malawi na Mweka Hazina wa SADCOPAC, Mark Botomani, aliwashukuru marais, Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuweka mazingira mazuri yaliyowezesha mkutano huo kufanyika kwa usalama na kwamba, Tanzania imekuwa mshirika muhimu wa Jumuiya ya SADC.

Kwa niaba ya wajumbe wenzake wa SADCOPAC, Botomani ameahidi kuwa watafanyia kazi mambo yote waliyojifunza katika mkutano huo ambao awali ulifunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia, wabunge, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na taasisi za ukaguzi kutoka nchi za SADC.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed




## Kinana asema serikali inafuatilia athari za mafuriko

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana amesema, Rais Samia Suluhu Hassan na serikali inafuatilia kwa karibu athari zinazotokana na mvua kubwa na kusababisha mafuriko na uharibifu wa miundombinu ya barabara na makazi ya watu.

Alisema katika maeneo yanayohitaji msaada wa dharura na haraka, serikali imeshachukua hatua ya kupeleka fedha za ukarabati wa miundombinu na misaada mbalimbali kuwasaidia walioathirika.

Kinana aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wanachama wa CCM Wilaya ya Musoma Mjini ambao walimweleza uharibifu wa baadhi ya miundombinu ya barabara katika wilaya hiyo na Mkoa wa Mara kwa kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

"Serikali inaendelea kufanya tathmini ya uharibifu huo wa miundombinu ili kutenga fedha za kukarabati maeneo yote ambayo yameathirika. Uharibifu wa miundombinu umefanyika katika nchi mbalimbali duniani hata zile zilizopiga hatua kubwa ya maendeleo na sio Tanzania pekee.

"Kwa mara ya kwanza tumeona duniani nchi nyingi zimepatwa na mafuriko, hata zile ambazo katika historia hazikuwahi kuona mvua, hivyo sio sisi peke yetu, haya yote yametokana na mabadiliko ya tabianchi, mahitaji ya kufanya marekebisho ni makubwa na yataendelea," alisema Kinana.

Alisema Rais Samia anapata taarifa kuhusu yote yanayotokea katika mikoa mingi, na sehemu ambako miundombinu imeharibika sana hadi kukosekana kwa mawasiliano hatua za dharura zimechukuliwa.

**MAENDELEO**

Kinana alisema Rais Samia anafanya mambo makubwa ya maendeleo kwa Watanzania ikiwamo kuongeza mapato ya serikali bila wananchi kushurutishwa au kuporwa fedha zao.

Pia, alisema chini ya uongozi wa Rais Samia nchi imepiga hatua kubwa ya maendeleo kuliko awamu nyingine zilizopita."Kwanini tusitoe pongezi kwa Rais Samia? Amefanya kazi nzuri, anajitoa, anajituma na kubwa amekuwa kiongozi wa mfano anaongoza nchi yetu vizuri na maendeleo yanapatikana kila mahali na Musoma hapa ni mashahidi.

"Hata katika ukusanyaji wa mapato hakuna mwaka tumepata mapato makubwa bila kufunga watu, bila kupora watu kama mwaka huu. Huu ndio ukweli, Watanzania tumuunge mkono, kuna usemi unasema ukitaka jambo lisemwe mpe mwanaume ukitaka lifanyike kwa uhodari mpe mwanamke.

"Chama hiki ni kizuri, ukiona hakiendi ujue wakubwa huku juu wanakivuruga, sio wanachama," alisema Kinana na kufafanunua kuwa serikali imejitahidi kupeleka maendeleo katika maeneo mbalimbali kwa usawa.

Hata hivyo, alisema shule ziko nyingi, maji yapo ya kutosha, hospitali ya kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere inaendelea vizuri na ujenzi, na kwamba Rais Samia amefanya mambo makubwa ya maendeleo.

# 'Majiji, miji hutumia gharama kubwa ulipaji fidia'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TATHMINI ya awali ya gharama inayohitajika kulipa fidia kwa mali zilizomo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara inapoongezwa ukubwa imeonyesha kuwa gharama kubwa zipo katika majiji na miji.

Naibu Waziri ya Ujenzi, Godfrey Kasekenya, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibaha Vijijini (CCM), Michael Mwakamo.

Mbunge huyo alihoji kuhusu mpango wa serikali kuepuka mzigo mkubwa wa ulipaji wa fidia wakati inapoongeza ukubwa wa barabara.

Akijibu, Kasekenya alisema wizara hiyo kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) imefanya tathmini ya awali ya gharama inayohitajika kwa ajili ya kulipa fidia kwa mali zilizomo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara lililoongezwa la mita 7.5 kila upande na kuonesha kuwa gharama kubwa za fidia ziko katika majiji na miji.

Alisema serikali inaangalia uwezekano wa kuchepusha barabara kwenye maeneo hayo.

Aidha, alisema uchambuzi wa kina unafanyika ili kubaini ni barabara zipi zinahitaji upana wa eneo la hifadhi ya barabara wa mita 60 kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya hapo baadaye ya kuzipanua kulingana na ongezeko la wingi wa magari na kazi hiyo itakapokamilika taarifa kamili itatolewa.

Awali, alifafanua kuwa serikali kupitia Sheria ya Barabara namba 13 ya mwaka 2007, iliongeza upana wa hifadhi ya barabara kutoka mita 45 hadi mita 60 kwa barabara kuu na za mikoa ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa miundombinu ya barabara kwa wakati huu na wakati wa baadaye ili uendane na ongezeko la watu na ukuaji wa shughuli za kiuchumi.

# TANROADS, TARURA wapatiwa bil. 136/- ukarabati miundombinu

**Na Vitus Audax,** DODOMA

WAKALA wa Barabara Nchini (TANROADS) pamoja na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) zimepatiwa Sh. bilioni 136 .2 kufanya ujenzi na marekebisho katika miundombinu iliyoharibiwa na mvua inayoendelea kunyesha nchini.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande, aliyasema hayo wakati akijibu hoja za wabunge kuhusu fedha ya dharura iliyopewa TARURA ili kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mvua, wakati wa uchangiaji katika bajeti ya TAMISEMI, mwaka 2024/25.

Chande alisema serikali inaendelea kufanya tathmini ya uharibifu mkubwa uliojitokeza katika wilaya na halmashauri zikiwamo barabara na madaraja.

Alisema serikali imechukua hatua za haraka ikiwa ni pamoja na kuipatia TARURA Sh. bilioni 61.3 pamoja na TANROADS ambayo imepatiwa Sh. bilioni 74.9.

Alisema fedha hiyo itaendelea kutolewa mpaka miundombinu itakaporejea katika hali yake ya kawaida.

"Niwaakikishie wabunge kwamba, fedha hii itatolewa kwa wakati kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika. Kuhusu ununuzi na kazi za nyongeza ya bajeti ya Sh. bilioni 350, suala hili Wizara ya Fedha tumekaa na wenzetu wa TAMISEMI na tumeelewana, mchakato wa ununuzi uanze ndani ya robo hii ya mwaka."

"Fedha hiyo itatolewa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha ujao ambapo itatumika ipasavyo katika ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja kama ilivyopangwa na sekta husika," alisema Chande.

Kuhusu TARURA kuongezewa nguvu kazi, Naibu Waziri wa OR-TAMISEMI sekta ya elimu, Zainab Katimba, alisema serikali imeshaajiri wahandisi 24 na katika mwaka 2024/25, tayari wameomba kibali cha ajira za wahandisi 97, huku wakiendelea kutumia wahandisi wanaofanya mafunzo kwa vitendo.

Alisema katika kukabiliana na vitendea kazi yakiwamo magari, serikali imetenga Shilingi bilioni moja.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, akizungumza wakati akifungua mkutano wa wahariri na waandishi wa habari ulioandaliwa na Wakala wa Usalama Kazini (OSHA), Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Huduma za Biashara, Netiwe Mhando na (wa pili kulia) ni Mkurugenzi Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# FAWETZ kuwezesha vijana 600 elimu vyuo vikuu

**Na Zanura Mollel**

SHIRIKA la Wanawake Waelimishaji Afrika Tawi la Tanzania (FAWETZ), linatarajia kuwezesha vijana wa elimu ya vyuo na vyuo vikuu 600 ikiwa asilimia 80 ni watoto wa kike na 20 wa kiume mwaka 2026 wanaotoka katika mazingira hatarishi kwa lengo la kuweka usawa katika nyanja ya upatikanaji wa elimu kwa makundi yote.

"Kila mwaka tutakua tunasomesha watoto 200 hivyo kwa miaka mitatu ya mradi wa kuwawezesha wanawake na wanaume kielimu na kujikomboa kiuchumi tutakua tumefanikiwa kusomesha 600," alisema Kitundu.

Mkurugenzi Mkuu wa FAWETZ, Neema Kitundu, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa ripoti ya utekelezaji wa Azimio la Itifaki ya Maputo, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi 44 za Afrika zilizokubali kutekeleza Azimio hilo.

Alisema serikali inatoa elimu bure kuanzia ngazi ya shule za msingi hadi kidato cha sita, lakini wapo wasichana wanaofaulu vizuri wanakutana na tatizo la kukosa ada kwa ajili ya kujiendeleza na elimu ya juu na kwamba wamejipanga kuwasaidia watoto hao.

"Tumeona tuwasaidie watoto wa kike asilimia 80 kwa kuwa bado wapo nyuma sana kwenye masuala ya elimu, wa kiume tutawasaidia asilimia 20, toka kuanza kwa jukwaa hili tumeshawasomesha zaidi ya watoto 5,000," alisema Kitundu.

Kwa kipindi cha miaka ya nyuma wasichana waliosomeshwa na shirika hilo walifikia malengo kwa asilimi 75 wengine walikabiliwa na changamoto ya mimba kipindi cha masomo pamoja na baadhi yao kujitambua wala kujithamini.

"Baada ya kulipuka kwa uugonjwa wa UVIKO-19 tulikosa fedha hivyo tukashindwa kuwafikia watoto wa kike katika msaada wa ufadhi wa masomo, hii ni changamoto iliyotusumbua sana," alisema.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Rajab Kangalawe, alisema kupitia Sheria ya Mtoto, mwaka ya 2009 ilipoanza kutekelezwa idadi ya watoto wa kike kwenye usajili ngazi ya msingi na sekondari imeongezeka kwa kiasi kikubwa.

"Mwaka 2009 idadi ya watoto wa kike waliosajiliwa kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha nne ilikua 627,041 huku wa kiume ikiwa 777,518 na kwa kidato cha tano na sita ilikuwa wanawake 26,377 na wanaume 38,388," alisema Rajab.

Alifafanua kuwa matokeo hayo ni dalili kuwa jamii imepokea elimu kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike, lakini pia jitihada za serikali kuweka mazingira rafiki ya ufundishaji kupitia miradi ya PEDP, SEDP, BOOST, EP4R, SEQUIP pamoja na Sera ya Elimu bila malipo.

"Mwaka 2023 wasichana waliopata elimu ilikua ni 1,608,202 na wanaume 1,469,153 Waraka wa Elimu wa mwaka 2020/21 Na.2 ulielekeza wanafunzi wote waliokatishwa masomo kwa makosa ya ujauzito na utoro kurudi masomoni isipokuwa wale wenye makosa ya jinai," alisema.

Alisema, serikali kwa kutambua umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike upo mfuko wa elimu unaotambulika 'Samia Scholarship' ambao husaidia watoto wa kike waliofaulu katika masomo ya sayansi.

"Malengo ya Azimio la Itifaki ya Maputo yamezingatia mahitaji, ukiangalia tumeweka elimu jumuishi kwa watoto wenye ulemavu (inclusive education) na kwa mwaka 2023 watoto wenye uhitaji maalum wenye uoni hafifu waliopo sekondari wa kike ni 3,517 na wakiume ni 2,494," alisema Rajab.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mwanaidi Ally Hamiss aliyataka mashirika yote yasiyo ya kiserikali (NGO's), yaliyopata usajili kutekeleza majukumu yao kama walivyobainisha katika usajili wake.

Alifafanua kuwa, serikali haitazifumbia macho mashirika yanayotekeleza majukumu yake nje na usajili na hatua moja wapo itakayochochukuliwa ni kufungia pamoja na kufuta usajili wake. "Wekeni nguvu pia kumkomboa mtoto wa kiume katika ukatili kutokana na mabadiliko ya kidunia."

"Nchi imekumbwa na vitendo vya kikatili, watoto wanabakwa jinsi zote tunapaswa kuondoa ukimya ili kutatua matatizo ya ukatili unaoibuka ndani ya jamii," alisema Mwanaidi.



# Wasiokuwa na vifaa kuhifadhi taka faini 50,000

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABISHARA wanaozalisha taka kwenye maeneo yao jijini Dodoma na wasio kuwa na vifaa vya kuhifadhia uchafu watalazimika kufungiwa biashara zao na kutozwa faini ya Sh. 50,000 hadi 300,000 kwa mujibu wa sheria ndogo za mazingira ya mwaka 2022.

Ofisa Afya wa Jiji la Dodoma, John Lungendo alitoa anagalizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara kutoka sekta mbalimbali baada ya kufanya ziara ya kuwaelimisha umuhimu wa kila mtu kuwa na chombo maalumu cha kuhifadhia taka kwenye eneo lake.

Akizungumza na wafanyabishara hao wakiwemo wa maduka,machinga,mama na baba lishe,hotelini na wajasirimali, Lugendo alisema watakaokutwa hawana vifaa hivyo jiji litalazimika kufunga biashara zao ikiwa ni pamoja kuwatoza faini hizo kwa mujibu wa sheria.

Alisema, pamoja na kuwaelimisha wafanyabiashara umuhimu wa kuweka vifaa hivyo, jiji halitasita kuwachukulia hatua za kisheria kwa wale watakaokutwa hawajatimiza agizo hilo la uwekaji wa vifaa.

"Jiji pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na watumishi wake wa idara ya afya, watendaji wa kata na mitaa na wadau wa mazingira, bado kuna wakaidi ambao maeneo hawaweki vifaa vya kuhifadhia taka hali inayobabisha kusambaa kwa taka ovyo, sisi kama jiji tutaendelea kuwachukulia hatua za kisheria," alisema.

Pia, aliwataka wafanyabiashara hao kutoka sekta mbalimbali ambao wanazalisha taka kushirikiana na wadau wa mazingira watumishi wa Jiji na vikundi vya kuzoa taka katika kushiriki zoezi la uondoaji wa uchafu ili mazingira yawe safi.

Awali, wakizungumza na waandishi wa habari kwenye uhamasishaji wa vifaa vya kuhifadhi taka, wafanyabiashara hao walisema Jiji la Dodoma bado linakabiliana na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kuzolea taka ikiwamo magari kwenye maeneo mbalimbali.

"Ili zoezi hilo lifanikishe kuna ulazima wa jiji kuongeza vifaa vyake ambavyo vitakuwa vikifanya kazi kwa muda wote, hii pamoja na kuongeza vikundi vya kuzoa taka pamoja na wafanyakazi kwa upande wa halmashauri hiyo ya Jiji la Dodoma," alisema.

Mathias Mtenga, Babalishe anayejishughulisha katika soko la wazi la Machinga, alisema Dodoma hivi sasa uzalishaji taka umeongezeka ni lazima kuwapo kwa vifaa vyakutosha ikiwamo magari, vikundi vya kuzoa na hata kwa wafanyakazi pia.

# 'Wakulima Kanda Kati wanazalisha chini ya kiwango'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Anthony Diallo, amesema wakulima wa Kanda ya Kati wanazalisha chini ya kiwango kutokana na dhana potofu waliyonayo ya matumizi ya mbolea kuharibu udongo wa mashamba yao.

Dk. Diallo alisema hayo juzi wakati akizungumza na wadau wa kilimo wa Mkoa wa Singida, ikiwa ni ziara ya wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya TFRA iliyolenga kutoa elimu na kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima.

Alisema, wakulima wengi hawataki kutumia mbolea kwa kudhani kuwa inaharibu udongo wa mashamba yao na kuamini kuwa itasababisha wavune mazao kidogo.

Dk. Diallo alifafanua kuwa ili wakulima waweze kuzalisha kwa tija na mazao mengi katika eneo dogo ni lazima wahimizwe kutumia mbolea kwa wakati na kwa usahihi na kwa kuzingatia ushauri unaotolewa na wataalam wa kilimo.

Aidha, Dk. Diallo aliwataka Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya kufuatilia taarifa ya afya ya udogo ya maeneo wanayoyasimamia ili wakulima watumie mbolea kulingana na mahitaji ya udongo wanaolima.

Alisema, taarifa hiyo pia itasaidia wazalishaji kujua aina ya virutubisho vinavyohitajika katika kila eneo la nchi na kuzalisha na kusambaza kiasi cha mbolea kinachotosheleza mahitaji husika.

"Huwezi kutumia mbolea bila kujua afya ya udongo, hivyo wakulima watumie kutokana na afya ya udongo wa mashamba yao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, alisema mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa imeendelea kuwa na matumizi madogo ya mbolea kutokana na mwamko mdogo na kusababisha wakulima kuzalisha chini ya kiwango.

Alisema ili kuongeza matumizi ya mbolea, aliwataka maofisa ugani kutoa elimu kwa wakulima kuhusu faida za matumizi ya mbolea ili waweze kutumia na kuongeza uzalishaji.

Kadhalika, aliahidi mamlaka hiyo kusimamia zoezi la kufikisha mbolea kwa wakulima kwa wakati ili kuondoa vikwazo vinavyoyowafanya wakulima kushindwa kutumia kwenye uzalishaji wao.

Baadhi ya wadau wa kilimo walioshiriki katika kikao hicho wameomba mbolea hizo ziwe zinawafikia kwa wakati ili kuwaepushia kadhia wanayoipata msimu wa kilimo unapofika na pembejeo hiyo kukosekana sokoni.



Baadhi ya wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, wakiwa wamembeba juu Mwenyekiti wa kanda hiyo, Mchungaji Peter Msigwa, baada ya wanachama wa Baraza la Wanawake la Chadema (BAWACHA) mkoa wa Mbeya kumpelekea fomu nyumbani kwake, mjini Iringa juzi, ili agombee tena nafasi hiyo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mradi waibua wenye maambukizi mapya VVU

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MRADI wa USAID Afya Yangu ambao unatekelezwa mkoani hapa umefanikiwa kuibua watu wapya zaidi ya 700 wenye maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na 600 wa kifua kikuu ambao wanaibuliwa kila baada ya miezi mitatu.

Meneja wa mradi huo Mkoa wa Singida, Said Mgeleka, alisema hayo jana wakati wa kikao cha kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi ambao umeanza kutekelezwa tangu Novemba 2021 katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Arusha, Tabora, Kilimanjaro na Singida.

Alisema wateja walioibuliwa kwa kugundulika kuwa na VVU wamesaidiwa kwa kuanzishiwa Dawa za Kufubaza Virusi (ARVs) ili wasiweze kupata madhara zaidi na kuilinda jamii na kama wasingeanza kutumia dawa hizo wanaweza kuwaambukiza watu wengine zaidi.

Mgeleka alisema kwa upande wa watu wanaoibuliwa wakiwa na ugonjwa wa kifua kikuu, wanasaidiwa matibabu na vipimo na baadhi yao wamepata ahueni na wengine kupona kabisa.

Alisema kwa upande wa uzazi wa mpango kila baada ya miezi mitatu mradi huo unawaibua zaidi ya wateja 1200 ambao hupatiwa njia za uzazi wa mpango za kisasa na pia katika kipindi hicho wanawake 1200 hufanyiwa uchunguzi kubaini kama wana viashiria vya ugonjwa wa saratani ya mlango wa uzazi.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, akifungua kikao hicho, aliwaagiza Waganga Wakuu wa wilaya na wadau wengine wa afya kuwatafuta na kuwarejesha katika matumizi ya dawa za kufubaza makali ya virusi vya Ukimwi waathirika 857 ambao wameacha kutumia dawa hizo.

Waathirika hao walioacha kutumia dawa za ARV wanatoka katika Halmashauri za Wilaya ya Ikungi, Singida na Itigi.

Dk. Mganga alionesha kutoridhishwa na idadi hiyo kubwa ya watu wanaotuma dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kuacha kutumia dawa hizo na amesisitiza kuwekwa mikakati na mipango madhubuti itakayosaidia kurejesha kundi hilo katika matumizi ya ARV dawa haraka iwezekanavyo.

Alisema kuna umuhimu wa kutengeneza mahusiano mazuri kati ya watoa huduma na wateja wao ikiwamo kuwapigia simu wanapoona mteja wao hafiki kuchukua dawa ili kujua sababu ambazo zinamfanya asiende kuchukua dawa hizo ili kuona namna bora ya kumsaidia.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Victorina Ludovick, ametaja sababu ya idadi kubwa ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI mkoani hapa kuacha kutumia dawa za kufubaza virusi kuwa ni waathirika hao kuhama na kwenda maeneo mengine na umbali kutoka kwenye makazi yao hadi kwenye vituo vya kutolea huduma hizo.

Ludovick alisema mpango uliopo kwa sasa ni kuhakikisha watumiaji hao wa dawa hizo wanatafutwa popote walipo na kuwapa ushauri nasaha kuhusu umuhimu wa matumizi ya dawa hizo kwa ajili ya afya zao.





# Kilimo cha mwani kuwekewa mkakati kuinua vipato

**Na Mwadishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema imejipanga kuendeleza njia za kitaalamu za ukulima wa mwani kuongeza uzalishaji pamoja na kuinua kipato cha wakulima wa zao hilo nchini.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Sudi Hamed, alisema hayo jana Muongoni, Mkoa wa Kusini Unguja wakati akikabidhi boti ya kuvunia mwani iliyotolewa na Taasisi ya The Nature Conservancy (TNC), inayoshughulika na utunzaji wa mazingira ya kimataifa ikiwa ni kuelekea shamrashamra za sherehe za Muungano ambazo hufanyika kila mwaka April 26.

Alisema zao la mwani linafaida kubwa katika ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja na taifa hivyo serikali itashirikiana na wadau wa maendeleo kutafuta njia mbadala za kuwasaidia wakulima wa zao hilo ili kujiongezea kipato.

Aidha, alisema moja ya mkakati wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, wakulima wanaongeza uzalishaji wa zao la mwani Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wakulima kuwafundisha njia za kitaalamu pamoja na kuwapatia vifaa vya kitaalamu lengo kuona wakulima hao wanafanya kazi zao kwa urahisi na njia za kitaalamu.

Aliwataka wakulima kutunza mazingira wakati wanapofanya shughuli za kilimo hicho ili kukabiliana na ma mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumzia kuhusu bei ya mwani, Mkurugenzi Salum alisema wizara inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani na ujenzi utakapomalizika wananchi watakuwa na sehemu maalum ya kuuza bidhaa ya mwani.

Mwakilishi kutoka taasisi ya TNC, Ayubu Misheli Singoye, alisema lengo la kutoa boti kwa wakulima wa zao la mwani katika Kijiji Cha Muongoni ni kurahisisha shughuli za uvunaji wa zao hilo wakati wa mavuno kwa wakulima.

Alisema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar kutoa elimu ya utumzaji wa mazingira ya bahari kuona shughuli za kilimo cha mwani hakiathiri mazingira ya bahari.

# Mwinyi aasa wananchi kuulinda, kudumisha Muungano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amesema ni wajibu wa kila mwananchi kuulinda, kuuimarisha, kuuendeleza na kuudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa dhamira ya Waasisi wa Taifa ili ulete mafanikio zaidi kwa vizazi vya sasa watakaokuja baadaye.

Aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi la ofisi ya Idara ya Uhamiaji katika Wilaya ya Mjini Unguja, ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za miaka 60 ya Muungano.

Alisema ni dhahiri kuwa jengo hilo litakapokamilika, litaongeza ari na kasi ya utoaji wa huduma za Uhamiaji katika mkoa huo wa Mjini Magharibi na manispaa zake zote tatu.

Alisema huduma za Uhamiaji zinahitaji kuzingatiwa katika kuimarishwa hasa ikizingatiwa kuwa Bandari ya Malindi kwa mwaka hupokea watalii zaidi ya 20,000 na uwanja wa ndege hupokea watalii zaidi ya 500,000 kwa mwaka.

Alisema kutokana na kasi hiyo ya uingiaji watalii, kunahitaji kuwa na jengo kubwa kwa Jeshi la Uhamiaji na majengo ya kisasa lenye vifaa katika kuwahudumia wageni na wawekezaji.

"Serikali itaendelea kuimarisha miradi mingine ikiwamo barabara, hospitali, shule ili kuweka mazingira bora ya utoaji wa huduma na kukamilisha mifumo ya utoaji wa huduma kwa njia za kieletroniki," alisema Dk. Mwinyi.

Naye Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Injinia Hamad Yussuf Masauni, alisema wizara yake inafarijika kuona mafanikio makubwa ya maendeleo katika miaka 60 ya Muungano katika nyanja zote.

Mbali ya udugu wa asili wa pande mbili hizo ulioasisiwa na viongozi waasisi wa Muungano ni kuimarisha usalama wa pande zote mbili.

Aidha, ana imani kukamilika kwa jengo hilo la Uhamiaji huduma kwa wananchi wa Zanzibar hasa wa Mkoa wa mjini Unguja zitaendelea kuiamrika.

Kabla ya Muungano, Uhamiaji hawakuwa na majengo ya ofisi, lakini sasa wana ofisi nzuri na serikali itaendelea kujenga ofisi katika wilaya zote kwa Zanzibar.

Alizungumzia changamoto katika mfumo wa mtandao kwa Zanzibar na kutoa wito kwa jeshi hilo kuendelea kuimarisha ufanisi wa kazi na viongozi kuwasimamia askari wa jeshi hilo waliopo katika malango makuu ya kuingia wageni na kufanya kazi kwa uadilifu na weledi.

Alisema askari wa jeshi hilo hawana sababu ya kutofanya hivyo kwa sababu mambo yote yanayostahiki kwao yamefanyiwa kazi ikiwamo kuwapa vyeo na kuongeza stahiki zao.

Alitaka kuona makusanyo na huduma zinatolewa haswa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ni kisiwa cha utalii na kwamba ni vyema kukusanya makusanyo vizuri katika malango makuu ya kuingia watalii ikiwamo viwanja vya ndege.

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Anna Makakala, aliishukuru Serikali ya Tanzania na Zanzibar kwa kuiwezesha Idara ya Uhamiaji kuwa na chuo cha mafunzo cha Uhamiaji, uimarishaji wa mifumo na majengo.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa jengo hilo, Kamishna huyo alisema utagharimu Sh. bilioni 9.9 na utachukua muda miezi 19 kukamilika Agosti, mwaka huu na mradi umefikia asilimia 55.

Alisema mradi huo unagharamiwa na Serikali ya Zanzibar na ukikamilika utaongeza tija na motisha kwa askari wa Uhamiaji kwa kuwekeza katika mazingira bora ya kazi.

"Tunaishukuru serikali ya Zanzibar kwa kutenga fedha Shilingi bilioni tano kwa ujenzi wa chuo cha mafunzo kinachotarajiwa kujengwa Kitogani Kusini Unguja pamoja na maandalizi ya ujenzi ofisi za Uhamiaji, Micheweni Pemba na katika Kisiwa kidogo Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini, Unguja," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Senga Guru, alisema wataendelea kushikamana na watendaji wote kufanya kazi kwa upendo katika pande ya Muungano ili malengo ya viongozi wakuu wa nchi yatimie katika kuimarisha Muungano.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma, alisema katika kero 18 ndani ya uongozi wa Rais Dk. Samia na Dk. Mwinyi, kero 15 zimeshatatuliwa na sasa zimebakia tatu.

"Hii yote inatokana na uongozi wenu uliobora ili wananchi wa pande zote mbili kunufaika na Muungano huu," alisema.



Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Jangwani, Dar es Salaam, Paulina Aweda (kulia), akionyesha tuzo aliyopewa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kutambua mchango wa shule hiyo kutunza na kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wakati walipowatembelea shuleni hapo juzi na kuwapa zawadi mbalimbali vikiwemo viti mwendo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yawekeza sekta afya kuimarisha huduma

**Na Mwandishi Wetu**

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, amesema, serikali imewekeza kwenye sekta ya afya, lengo ikiwa kuimarisha huduma hiyo kwa maendeleo ya taifa na wananchi wake.

Aliyasema hayo jana wakati wa uwasilishaji wa matokeo ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria mwaka 2022 kwa maofisa wa afya na mipango mikoa na wilaya, mjini Unguja jana.

Aliwataka maofisa hao kuyatumia vizuri matokeo hayo ili yawe na tija kwenye sekta ya afya, ikiwamo kutatua changamoto za vifo vya mama na mtoto.

Alisema, Serikali ya Awamu ya Nane imefanya uimarishaji mkubwa sekta ya afya, changamoto za vifo vya mama na mtoto ziepukike kwa kutumia matokeo ya utafiti huo.

"Matokeo hayo yaje na mageuzi chanya kisekta na hilo linawezekana ikiwa kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake," alisema.

Aidha, aliwataka maofisa hao ambao wengi wao wakiwa wataalamu wa afya, kutambua vifo vinavyotokana na uzazi vinavyochangia kupunguza nguvu kazi ya taifa na kwamba wanatakiwa kuviepusha.

"Baada ya mafunzo haya mkalete mageuzi ya kweli kwenye maeneo yenu," alisisitiza na kuongeza kuwa utafiti huo una umuhimu wa pekee ndani ya jamii na taifa.

Alisema taifa lolote haliwezi kuwa na maendeleo kama litakabiliwa na changamoto ya wananchi wake kukosa afya bora.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema, ni dhahiri kuwa matokeo hayo yanatokana na juhudi mbalimbali zinazoendelea kufanywa na serikali katika kuwaletea wananchi huduma bora za afya na zilizo karibu na maeneo wanayoishi.

Mratibu wa Huduma za Afya ya Mama na Mtoto Mkoa wa Mjini Magharibi, Saida Abubakar Mohammed, alisema, utoaji wa huduma mbalimbali za afya ikiwamo huduma kwa mama na mtoto ni jambo linalopewa kipaumbele.

Hata hivyo, alisema zipo changamoto mbalimbali zinazowakumba hasa wajawazito ikiwa ni pamoja na kuchelewa kufanya uamuzi wa kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kupata huduma.



**MOBETO**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
UDANI TELE





# KUMBE 'NANUSU' ndio sababu......

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Harmonize, hatimaye ametambulisha ngoma yake mpya 'Nanusu', baada ya wiki moja kuibua mjadala mkali kutokana na kauli yake tata kuhusu uumbwaji wa mwanamke.

Kauli hiyo ya Harmonize iliyoonekana kama kumfananisha mwanamke sawa na Mungu, ilipokelewa kwa hisia tofauti kiasi ambacho baadhi ya viongozi wa dini walimtaka msanii huyo kuomba radhi.

Hata hivyo, jana alitambulisha ngoma hiyo Nanusu na kuelezea kwamba ni maalum kwa wanawake wote duniani kwa ajili ya kuwapa moyo katika changamoto mbalimbali za kimaisha wanazopitia.

"Wimbo huu ni maalum kwa wanawake wote duniani, nikiwa kama baba wa mtoto wakike nina kila sababu ya kumjengea binti yangu hali ya kujiamini kuwa anaweza kufanya chochote au kuwa yeyote endapo atapata nafasi na kuweka mchango mkubwa katika jamii,"

Katika ujumbe wake huo amesema anaamini katika kufanya hivyo kutakuwa na mashujaa wengi wanawake na kumtolea mfano Rais Samia Suluhu Hassan.

BASI SAWA

## P Funk ataka wajukuu wengi kwa Paula



MTAYARISHAJI mkongwe wa muziki nchini, P Funk amewataka vijana wake Marioo na Paula kutokuwa wavivu kwani anatarajia kupata wajukuu zaidi ya mmoja  katika maisha yao.

P Funk ametoa kauli hiyo wakati akiwapongeza katika hafla ya kuwapongeza kwa kutarajia kupata mtoto wao wa kwanza hivi karibuni.

"Omari (Marioo) ninakuombea uwe baba bora na uwe mume bora, nataka muwe na watoto na sio mtoto mmoja kwenye ndoa yenu," amesema P Funk.

## Octopizzo afurahia mabifu

RAPA mkali kutoka Kenya, Henry Ohanga, almaarufu Octopizzo, amesema bifu kati yake na msanii mwenzake Brian Auko Omollo, maarufu kama Jones, imewaingizia pesa nyingi.

Akizungumza hivi karibuni, Octoipizzo, amesema katika ulimwengu wa muziki hip hop tofauti za wasanii ni moja ya njia ya kutafuta pesa, lakini nyuma ya pazia kuna maelewano mazuri.

"Huyo ni morio ni wangu na azidi kuweka bidii. Pigamawe," amesema Octopizzo alipoulizwa kama wawili hao wana uhusiano mzuri nje  ya           muziki.





# HAMISA MOBETTO AMWAGA UGALI

Mwanamuziki na mwanamitindo maarufu nchini Hamisa Mobetto, ameamua kumwaga ugali kwenye kundi la watu, baada ya kuliondoa jina la Diamond katika utambulisho wa mtoto wake wa kiume Dylan.

Mobetto, ambaye ni mama wa watoto wawili, amebadilisha jina la utambulisho wa mtoto wake huyo katika mtandao wa kijamii na sasa anajulikana kama Dylan Mobetto, ikidaiwa ni jibu tosha kwa mzazi mwenzake Diamond Platnumz ambaye  inaonekana hajamkubali.

Hata hivyo, Hamisa aliamuacha binti yake kuendelea kutambulika kama Fantasy Francis, ikielezwa inatokana na kuwa na uhusiano mzuri na baba wa mtoto huyo Mojito Francis.



## Baba levo alikoroga tena

MWANAMUZIKI na mtangazaji maarufu nchini, Baba Levo, ameibua mjadala baada ya kuweka hadharani majeraha aliyoyapata baada ya kupigwa na mkewe Mama Ruby.

Baada ya kuweka picha katika ukurasa wake wa Instagram, inayoonyesha michubuko sehemu ya mabegani na mbele ya kifua akidai yanatokana na kipigo, baadhi ya mastaa waliotoa maoni yao wamemshauri kutulia kwa sababu kila mtu anapitia matatizo mbalimbali.

Msanii wa filamu, Mwijaku alikwenda ,mbali kwa kueleza kwamba matatizo anayoyapata Baba Levo yanatokana na tabia yake ya kutoka nje kimapenzi huku akijua ana mke nyumbani anayeweza kutimiza majukumu yake.

FILAMU

# Sikitu: Leo mboga kesho sumu

**Na Adam Fungamwango**

BINADAMU siku zote ni kama mboga aina ya uyoga. Ukienda kuchuma unabidi uwe mwangalifu kwa sababu kuna uyoga mwingine unakuwa ni sumu.

Ndivyo alivyo binadamu, leo anaweza kuwa mwema kwako, lakini kesho akawa adui. Ni kama tu mboga ya uyoga, leo inaweza kuwa mboga, lakini kesho ikawa sumu.

Ukitaka kuthibitisha hili hebu soma filamu hii ya kusikitisha iitwayo, 'Sikitu' au itafute na kuiangalia.

Imechezwa na Kajala Masanja, Hemed Suleiman, Taira Odera, Matra Taimamu, hayati mzee Majuto, Tausi Mgendela, Asha Boko na wengineo wengi.

Hemed na Kajala ambaye amecheza kama Sikitu ni mke na mume. Ni watu wenye uwezo na wanaishi maisha ya kifahari.

Sikitu anapatwa na ugonjwa unaomfanya ashindwe kufanya chochote kile. Hemed anaamua kumrudisha nyumbani kwao kwa ajili ya matibabu, pia kupata muda wa kupumzika.

Hata hivyo, Hemed anaingia kwenye penzi na mdogo wa mkewe, Taira. Penzi hilo linakuwa moto moto hadi inakuwa si siri tena. Wazazi pia wanafahamu hilo. Wanawaita na kuwakanya, lakini inakuwa ni kazi bure.

Sikitu anagundua hilo. Anapatwa na mshtuko wa moyo unaosababisha kupooza mwili. Hatimaye anakata roho.

Hemed na Taira wanakwenda msibani, mzee Majuto ambaye ni baba wa mabinti wote wawili, Sikitu na Taira, kwani wamesababisha kifo cha binti yake.

Wanarejea nyumbani kwao mjini kuendelea na maisha yao ya kawaida.

Siku isiyo na jina, majambazi wanavamia nyumbani kwa Hemed. Wanataka wamuonyeshe alipoweka hazina ya pesa. Wakati mwenyewe Hemed akisuasua, Taira aliwaonyesha majambazi mkoba wa pesa ulipo.

Kwa mastaajabu, majambazi baada ya kuchukua mkoba ule,  wanamkabidhi mmoja wa watu ambao wamewaweka chini ya ulinzi, si mwingine ni Taira.

Ananyanyuka na kuchukua mkoba wa pesa, akamgeukia Hemed na kumwambia hakuwa na mapenzi ya kweli, badala yake alikuwa anazitaka zile pesa tu. Bastola aliyokuwa nayo mkononi ilitosha kumtoa uhai Hemed. Wakati wale majambazi wakidhani watalipwa ujira wao kwa kazi ile, Taira akawageukia nao kwa risasi, wote na kuwa maiti.

Tayari Taira akajiona mshindi kwani ni yeye tu aliyebaki hai ndani humo, alichotaka amekipata, akatoka ndani ili atokomee kusikojulikana.

Kumbe mdogo wa Hemed, Matra alikuwa amefika nyumbani hapo na kushuhudia mchezo mzima.

Wakati Taira anatoka, Matra alinyanyua kistuli na kumpiga nacho kichwani, akapoteza maisha hapo hapo. Mkoba wa pesa ukawa mikononi mwa Matra, mdogo wa Hemed ambazo alizipeleka kwa wazazi wake. Urithi ukarudi nyumbani.




# DIBLO, DALLY, WALIVYOTESA WABONGO

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 1990, kulikuwa na mapinduzi ya muziki nchini Congo DR, ambayo wakati huo bado ilikuwa ikiitwa Zaire.

Muziki wa rhumba, na Cavasha ulidorora, ukaja aina fulani ya muziki ya mapigo ya kasi. Yalifanana kiasi na ya Cavasha, lakini yenyewe yaliongezewa vionjo fulani kama, ikiwa pia hatua aina ya uimbaji haikuwa ya muda mrefu sana. Waimbaji waliimba kwa dakika kadhaa tu, lakini uimbaji uliokuwa wa kuvutia sana, ila sebene ndiyo ilikuwa inaachiwa inatawala kwa muda mrefu. Wakaupa jina la muziki wa soukous.

Gitaa ongozi, au gitaa la solo, ndilo lililoongoza zaidi muziki huo.

Kwenye magitaa ya solo ndiko kulikokuwa na ushindani zaidi. Na ndiko mashabiki wengi wamuziki Afrika, ikiwemo Tanzania walikuwa wanapenda zaidi.

Na karibuni wapiga magita wote hao hawakuwa na bendi rasmi. Walikuwa wakikodishwa na bendi, makundi au wanamuziki mbalimbali waliowahitaji. Hapa nitawataja wapiga solo waliojizolea umaarufu sana hapa nchini kutokana na upigaji wao kuwakuna wengi.

**Diblo Dibala**

Huyu ndiye alikuwa kipenzi zaidi cha mashabiki wa muziki Bongo miaka ya 1990 kwenye muziki wa soukous. Upigaji wake kama vile gitaa liko kwenye maji, uliwafurahisha na kuwashangaza wengi. Diblo ambaye ni zao la TP OK Jazz chini ya Franco ambaye miaka ya 1970, alifanya shindano ya kuibua vipaji yeye kushinda. Hakujulikana sana hadi yeye pamoja na marehemu Arlus Mabele walipounda kundi ya Loketo.  Alipiga solo nyimbo kama 'Extra Ball', lakini baadaye alijiuengua na kwenda kuunda bendi yake ya Matchatcha. Kwenye bendi ya Empire Bakuba ya Pepe Kalle, aliga solo kwa ufundi wimbo wa 'Pon Moun Paka Bouge'.

**Dally Kimoko**

Ni mpiga solo aliyependwa sana si na mashabiki wa muziki huo Afrika, bali hata na wanamuziki wengi walipenda kufanya naye kazi. Solo lake lilichezeka zaidi na kuwa kwenye mahadhi ya Kiafrika.

Hata mwanamuziki wa Zouk, marehemu Oliver Ngouma alifanya naye kazi.  Karibuni kwenye kila wimbo ambao anaupiga kwenye makundi mbalimbali, mama Soukous Stars, Yondo Sister, Madilu System, Loketo Group na mengine mengi na kote huko, hawakukosa kumtaja kwa kusema 'Dally Kimoko, gitare zanga likwanza'. Maana yake ni kwamba Dally Kimoko, gita lisilokuwa na mikwaruzo.

Amepiga nyimbo nyingi sana ambazo hata hapa hazitoshi kuziandika, lakini kwenye bendi Pepe Kalle alipiga gitaa kwenye wimbo maarufu sana nchini 'Shikamoo Seye', Wabongo wanauita 'Hidaya'. Msikilize pia kwenye 'Inde Monie' ya Kanda Bongoman.

**Benico Ipopolipo**

Naye hakuwa nyuma kwenye upigaji wa solo. Ni mwanamuziki aliyekuwa kwenye bendi ya Zaiko Langalanga, lakini alikuwa akikodiwa kwenye makundi mbalimbali ya muziki nchini Congo DR.

Mkono wake wa gitaa la solo unajieleza kwenye nyimbo za Pepe Kalle kama 'Roger Milla', 'Gerant', na 'Zonga Aime,' ambazo zilipendwa sana na Watanzania. Humpagawisha sana Pepe Kalle mpaka anamwita 'Beniiicooo.' Amepiga solo pia kwenye nyimbo nyingi za Madilu System.

**Nene Tchakou**

Mmoja wa wapiga solo wazuri kabisa nchini Congo DR, waliofanya vema kwenye muziki wa soukous.

Huyu alipiga nyimbo nyingi za Kanda Bongoman, Yondo Sister, Soukous Stars na makundi mengine.

Amepiga nyimbo nyingi, lakini ukitaka kumfaidi sikiliza 'Isambe' ya Kanda Bongoman. Hadi anaitwa 'Tchakutchakutchaku baba ooo ooo'.

**Caen Madoka**

Caen Caen, Caen Madoka, anasikika hayati Aurlus Mabele akimtaja kwenye kibao ya Khadija' na zingine alizopiga akiwa na Loketo Group. Ni miongoni na wapiga gitaa la solo aliyepigia makundi mbalimbali wakati wa soukous na kufanya vema, akijipatia umaarufu na kualikwa huku na kule.



# Bibi kumpatia mtoto Serengeti boy wake

MWIGIZAJI na mwandishi mkongwe wa Colombia, Alina Lozano Acosta, mwenye umri wa miaka 55, ameibua mjadala baada ya kutangaza kuwa mjamzito wa mpenzi wake Jim Velasquez, ambaye ni mdogo kwa miaka 31.

Wawili hao ambao ni walifunga ndoa miezi michache iliyopita, walitangaza kuwa wanatarajia kupata mtoto wao wa kwanza.

Wanandoa ambao wamekuwa kivutio kutokana na maisha yao binafsi kwenye mitandao ya kijamii, wamekuwa wakipuuza maneno ya chuki kutoka kwa watu mbalimbali.



## Ruger kwa hili sio sawa

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Ruger, amesema hawezi kujilaumu kutokana na ujumbe wake aliouchapisha ukurasa wake wa X, ambao wengi wanauona kama unaunga mkono ubakaji.

Akiwa mwenye hasira na lebo yake ya zamani ya Jonzing World, ambayo ilihamasisha upingaji wa ujumbe huo, amesema hajilaumu na hawezi kuomba radhi.

Katika ujumbe wake msanii huyo aliandika maneno ambayo yanawatahadharisha wanawake wanaotaka kupanda boti lake hawatarudi salama.

## Dj Switch yamemkuta

MCHEZA muziki wa Nigeria, Obinuju Catherine Udeh, maarufu kama DJ Switch, amekanusha madai kwamba alikamatwa na polisi kama ilivyoripotiwa na mtandao mmoja wa udaku.

Katika chapisho aliloandika kwenye mtandao wa X (zamani Twitter), DJ Switch alisema madai yote yakiwemo kwamba alimshambulia polisi wa kike katika kituo cha polisi yalikuwa ya uwongo.

"Niliamshwa na simu na meseji nyingi asubuhi ya leo, nikajiuliza kwanini kwa sababu najua haikuwa siku yangu ya kuzaliwa, nikakuta taarifa eti nimekamatwa. Mimi si shabiki wa polisi wetu wengi wanaume na wanawake, siungi mkono unyanyasaji dhidi ya polisi," amesema.





## Ifeoma kwani ulimpataje Okoye?

MREMBO Ifeoma Ivy, ambaye ni mpenzi wa mwimbaji wa kundi la P-Square, Paul Okoye, amekanusha kwamba yeye ndiyo chanzo cha kupewa talaka kwa Anita Okoye.

Kupitia ukurasa wake mubashara wa Instagram, Ivy amesema alichumbiana na mwimbaji huyo baada ya Anita kupewa talaka na kwamba hahusiki na kuachana kwao.

"Sio lazima nifanye hivi hata kidogo, lakini sijawahi kusema neno lolote kuhusu hilo na inaonekana wengi wenu wamezoea habari za uwongo. Nilikutana na Paul akiwa mwanaume singo,"amesema

## Cavill wa Superman sasa anaitwa baba

MWIGIZAJI wa filamu za Superman, Henry Cavill, anatarajia kupata mtoto wake wa kwanza na mpenzi wake, Natalie Viscuso, ambaye ni mtendaji mkuu wa Hollywood.

Wanandoa hao, ambao wamekuwa katika uhusiano kwa miaka mitatu, walishirikisha taarifa hiyo kwa wafuasi wao kupitia mtandao wa Access Hollywood.

Akielezea furaha yake, Cavill amesema yeye na Natalie wote wanafuraha kwa kumpata mtoto huyo na wamemtabiria ataona mengi ya wazazi wake.





## Waziri Silaa kupiga kambi Tanga, kusikiliza kero ya ardhi

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amepanga kupiga kambi ya siku saba katika Mkoa wa Tanga, kuwasikiliza wananchi wenye migogoro kupitia kliniki ya ardhi itakayofanyika kuanzia Aprili 22 hadi 28, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa mkoa huo, Tumaini Gwakisa, Silaa, ataanza kupita kwenda mguu kwa mguu eneo la kijiji cha miaka 21 kilichoko Kata ya Chumbageni na baadaye kuhamishia kliniki hiyo Wilaya ya Korogwe.

"Katika Jiji la Tanga, Waziri mwenye dhamana atasikiliza migogoro ya ardhi, nyumba na makazi kati ya Aprili 22 mpaka 25, mwaka huu.

"Baada ya kumaliza Jiji la Tanga, ataelekea Korogwe ambako ataendelea na kliniki hiyo kati ya Aprili 26 mpaka 28, mwaka huu; na uendeshwaji wa programu hiyo itaongozwa na Waziri wa Ardhi akiwa na wataalamu wa wizara hiyo.

"Nichukue nafasi hii kuwaalika wananchi wote wa Tanga, kuhudhuria na kupata huduma mbalimbali za sekta ya ardhi katika maeneo ambayo kliniki hiyo itafanyika."

"Kliniki hii ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anataka kusogezwa kwa huduma kwa wananchi wetu. Sasa huduma imesogezwa tayari.

"Mwenye changamoto yoyote ile ya ardhi ikihusisha kupata hati, migogoro katika maeneo yetu ambayo inasababisha kushindwa kupata hati hapo, ndio eneo sahihi.

# Jela miaka 20 kosa kukutwa na meno ya tembo

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MKAZI wa Kijiji cha Masandare, Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Said Mshana (45), amehukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani kwa kosa la kukutwa na meno ya tembo.

Mshana, alikuwa akikabiliwa na makosa mawili ya uhujumu uchumi, ambayo ni kukamatwa na nyara za serikali kinyume na sheria na kujihusisha na ujangili wa nyara za serikali.

Makosa hayo ni kinyume na kifungu cha 86 (1) na (2) (b) vya Sheria ya Wanyamapori, Namba 5 ya Mwaka 2009, ikisomwa pamoja na aya ya 14 (1) 57 (1) na 60 (2) ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 iliyofanyiwa Marejeo mwaka 2019.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mkuu, Chrisanta Chitanda, alisema mahakama imejiridhisha pasipo shaka kwamba, mshitakiwa alikamatwa katika eneo la Kandoto, Kata ya Kisima, akiwa na meno sita ya tembo yenye uzito wa kilogramu 33, yenye thamani ya Dola za Marekani 45,000 (sawa na Sh. milioni 105.255 za Tanzania).

Kwa mujibu wa Hakimu Chitanda, kosa la kwanza lililokuwa likimkabili Mshana ni kinyume na kifungu cha 86 (1) (2) (C), Sura ya 283 ya Sheria ya Wanyamapori iliyofanyiwa Marejeo ya mwaka 2022.

Kosa la pili ni kinyume na kifungu cha 84 (1) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022.

Kabla ya hukumu hiyo, Mwendesha Mashitaka wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Samweli Magoko, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshitakiwa ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo.

Alidai kuwa makosa aliyoyatenda mshitakiwa huyo kwa mujibu wa sheria ni makosa ya uhujumu uchumi na yanafubaza jitihada za serikali katika kulinda na kuhifadhi rasilimali za nchi, kwa manufaa ya Watanzania wote.

Katika hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Magoko, alidai kuwa Februari 28, 2023 katika eneo la Kandoto, Kata ya Kisima, mshitakiwa alikamatwa na maofisa wanyamapori, baada ya kumuwekea mtego, wakimhadaa kwamba wao ni wanunuzi wa meno ya tembo, ambapo mshtakiwa alijitokeza na kuwaonyesha meno hayo ya tembo aliyokuwa nayo.

Nje ya mahakama hiyo, Kamisha Msaidizi wa Uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa Mkomazi, Emmanuel Moirana, alitoa rai kwa wananchi wote wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu wa namna hiyo, kuacha mara moja kwa kuwa Jeshi la Uhifadhi kupitia Kitengo cha Intelejesia na Upelelezi, vimejipanga kukabiliana na uhalifu wowote wa nyara za serikali unaotokea ndani na nje ya hifadhi.




Mbunge wa Jimbo la Hanang', mkoani Manyara, Mhandisi Samwel Hhayuma (kushoto), akizungumza na wataalamu wa nishati kuhusu namna ya kuwashirikisha na kuwanufaisha wapiga kura wake, alipotembelea maonyesho ya nishati, katika mji mdogo wa Katesh, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC awaonya viongozi kunyanyasa walio chini yao

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Fakii Lulandala, amewaonya wakuu wa idara wa halmashauri hiyo wenye tabia ya kutumia nafasi zao kuwakanyaga na kuwanyanyasa watumishi wengine walioko chini yao kuacha mara moja.

Amesema ikibainika wapo wanaoendelea kutumia vyeo vyao kuwanyanyasa wengine, atawashughulikia pasipo kuangalia wanafahamiana na kiongozi gani wa juu serikalini.

Lulandala alionya kuhusu hali hiyo jana, akiwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Orkesumet, wilayani humo.

Kutokana na malalamiko ya aina hiyo kuripotiwa mara kadhaa katika wilaya hiyo, aliwataka watumishi wa umma kutumia nyadhifa walizopewa serikalini kuwahudumia wananchi kwa umakini, unyenyekevu na uadilifu wa hali ya juu.

Katika hafla hiyo ya kumuaga Mkuu wa zamani wa wilaya hiyo, ambaye kwa sasa ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Suleiman Serera, alisema sasa hivi yuko kwenye wizara ya furaha.

"Kule tupo kwenye furaha, hatuna msongo wa mawazo, wala malalamiko ya basi limegonga mifugo ya wafugaji wanakuja kukulalamikia hakuna," alisema Dk. Serera.

"Watumishi msijione wanyonge kuwapo Simanjiro. Simanjiro inaangaliwa kwa jicho la kipekee, fanyeni kazi kwa bidii na siku moja mtaonekana na kutambulika zaidi ya hapo mlipo," alisema Dk. Serera.

Awali, Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Warda Abeid Maulid, alisema watamkumbuka Dk. Serera kwa misimamo yake mikali alipokuwa akiwaongoza.

"Tutakukumbuka kwa mambo mengi ikiwamo kupenda uwajibikaji, ukweli na kutatua migogoro ya jamii ya eneo hili," alisema Warda.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Misiba ya sasa, ukilinganisha na zama zile, imebadilika kupitiliza!

Na Adam Fungamwango



MIENENDO ya watu siku hizi misibani imebadilika kabisa, siyo kama ilivyokuwa zamani.

Kuna tofauti kubwa utaikuta siku hizi katika misiba, kuanzia kwa wafiwa, majirani, ndugu, mpaka waombolezaji.

Sababu zipo, lakini inavyoonekana moja wapo ni athari za maendeleo ya teknolojia.

Kwanza, miaka ya nyuma eneo lenye msiba lilitisha watu wengi kiasi kwamba hata baadhi ya watoto waliogopa kupita. Wasichana ambao hawakuhusika kabisa, ambao huwa wanapita tu, walibadilisha kabisa njia.

Siku hizi kwenye msiba, watu wamekaa, lakini wanapita bila matatizo yoyote, tena kwa madaha.

Ilikuwa mama zetu wakisikia msiba, atatoka amefunga khanga, anafunga kilemba na kuvaa kandambili zake, kihuzunihuzuni!

Majirani wanapofika msibani kitu cha kwanza ni kumfariji mfiwa, kuchukua watoto wake wote wenye umri mdogo na kuwaondoa eneo la tukio, wakipelekwa nyumba jirani ambako watafanyiwa kila kitu, wataoga, watakula na kuambiwa wakae ndani na wenzao.

Majirani wa kike watakutana na kupanga nini cha kufanya, ambapo kila mmoja ataingilia huku na kuleta unga, mchele, sukari, kuku, bata, pamoja na kutafuta kuni za kupikia, ili kumpunguzia gharama mfiwa, ambaye wakati huo, akili yake haijakaa sawa kutokana na pigo la kufiwa.

Kikubwa zaidi ni kwamba muda wote watakuwa na mfiwa, wakihakikisha halii moja kwa moja, badala yake kumbembeleza kula chakula, na mahitaji mengine muhimu ili aendelee kuwa na nguvu.

Wanaume majirani nao wataitana kuhakikisha mwenzao anatatiwa kila aina ya msaada ya awali kabla ndugu na jamaa hawajafika, ikiwemo kupitisha michango, na mengine yanayofanana na hayo.

Kifupi ni kwamba zamani utawasikia waombolezaji muda wote waakimlilia marehemu, wakitoa michango mbalimbali. Wapo waliokuwa wakisaidia kazi muhimu msibani, wengine wanawatia moyo wafiwa.

Wapo wataohakikisha mali za mrehemu na vitu mbalimbali pale nyumbani haviibiwi kwa sababu wafiwa wanakuwa hawapo kwenye hali ya kawaida, nyuso za zao zilionekana kuwa na simanzi kiasi kwamba mtu unapopita huwezi hata kuuliza kama kuna msiba au la, pia watu wanaswali, wanasali na kuimba kwa hisia kali.

Kinyume chake, mienendo ya watu misibani siku hizi inahuzunisha kuliko hata msiba wenyewe.

Msiba ukitokea, utawasikia waombolezaji wakidodosa kinachoendelea au ratiba imekaaje, ili wahudhurie tendo la mwisho ambalo ni kuzika, watawanyike. Ni adimu siku hizi kusikia siku tatu za msiba baada ya kuzika.

Hapo msibani watu wanaendelea na maisha ya kawaida, wanaongea mpira, wanataniana, wanabishana, wengine wanachati na simu mwanzo, mwisho, hakuna tofauti na mtu anavyoshinda sebuleni kwake, kama vile hakuna chochote kilichotokea. Simu ziko bize kupiga picha na kuziposti kwenye akaunti zao.

Walio machachari, tayari wameshakuwa wenyeji kwenye 'pub', za jirani na hata kuzama kwenye maasi, baada ya kumalizika msiba unasikia mengi yatokanayo, kupitia umbea wa mtaani.

Wanaolala msibani hivi sasa ni wale wanandugu hasa, damu damu na marehemu, au ambao hawana pesa, lakini ndugu wengine visingizio vingi, ili mradi tu asishinde hapo.

Kipengele cha kulala msibani, ndiyo kimebadilika balaa. Huwezi amini, kwa sababu hizio hizo, kundi kubwa linajaa gesti za jirani, huku wengine usiku kucha kama hawako 'pub', basi kwenye mechi za Arsenal, na haishangazi simulizi za ndoa nyingi huanzia kwenye matukio hayo.

Huko uani, kinamama wanashindana nani kaja na dela la gharama, na simu ya bei mbaya, ndugu yangu kama umekuja na kitochi, utakoma.

Kuna wafanyaji tathmini, mara yupo jikoni, kisha kaenda sebuleni walipo wafiwa, akirudi huko, mjadala ulioshiba. Vile vile waliomo na wasiomo kwenye umbea, kila mtu kaweka antena, 'marehemu kafa kwa nini?' Atasemwa marehemu, mwenza wake, wanandugu wote, mpaka unajiuliza, wamekuja kulia, au wana jambo lao? Hapo nimemsahau mmoja, mtaalam kakusanya kundi hilo, yeye ndiyo anamjua marehemu ndani , nje, akimfafanua kama vile mwanahabari aliyekabidhiwa jukumu hilo, akaliambie umma.

Yaani, kila nililitafakari hili naishia kujiliwaza, makubwa haya, mbona madogo yana nafuu!

**Tuma meseji 0716 350534**



## HABARI KIMATAIFA

# Israel yaishambulia Iran, hofu yatanda kila sehemu

**TEHRAN,** IRAN

USIKU wa kuamkia jana taifa la Iran lilikabiliwa na shambulizi la kulipiza kisasi yaliyojumuisha kombora na ndege zisizo na rubani kutoka kwa Israel.

Vyanzo mbalimbali viliripoti kuwa Israel ilifanya shambulio hilo la kulipiza kisasi ndani ya ardhi ya Iran, siku chache baada ya nchi hiyo kushambuliwa kwa makombora na ndege zisizo na rubani 300 na Iran.

Milipuko ilisikika katika mji ulioko katikati ya nchi hiyo wa Isfahan, lakini serikali ya Iran ilieleza hakuna athari yoyote iliyotokea.

Ofisa mmoja wa Iran aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba milipuko hiyo ilisababishwa na mifumo ya ulinzi wa anga ambayo ilifanikiwa kudungua droni tatu.

Hata hivyo, viongozi wa serikali ya Israel na jeshi hawajazungumza chochote kuhusu taarifa hii.

Ofisa mwandamizi wa Iran ameiambia Reuters kuwa nchi pamoja na shambulizi hilo, ofisa huyo wa Iran alisema nchi yake haina mpango wa kujibu mara moja shambulio hilo ambalo halikuwa na madhara makubwa.

Chanzo kinachofuatilia mgogoro huo kilieleza kuwa Marekani ilipokea taarifa kabla ya Israel kufanya shambulio hilo, ambalo limefanyika siku chache baada ya Iran kuendesha mashambulizi ya droni na makombora ambayo hayajawahi kushuhudiwa dhidi ya Israel.

Kwa upande mwingine, Shirika la Kimataifa la kudhibiti Nishati ya Atomiki (IAEA) lilisema shambulio hilo halijasababisha uharibifu wowote katika miundombinu ya nyuklia ya Iran.

Aidha, ilikumbusha kwamba nchi zote mbili kuwa maeneo yenye miundombinu ya nyuklia hayapaswi kulengwa katika mgogoro huo.

Maofisa wawili wa Marekani waliambia vyombo vya habari kwamba shambulio hilo lilifanywa na Israel, lakini nchi hiyo haijasema chochote kuhusu tukio hilo.

Wakati huo huo, nchi ya Oman imelaani shambulizi hilo lililofanywa Iran.

Katika taarifa kutoka kwa wizara ya mambo ya nje, ilisema nchi hiyo imelaani mashambulizi ya mara kwa mara ya jeshi la Israel katika eneo hilo.

Oman imekuwa ikifanya kazi kama mpatanishi katika mgogoro wa Mashariki ya Kati ikijaribu kuondoa hali wasiwasi iliyotanda eneo hilo.

Serikali ya Ufaransa pia ilitoa wito wa kupunguzwa kwa uhasama katika eneo hilo.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean-Noel Barrot, alisema msimamo wa nchi yake ni kutaka wahusika wote kupunguza kasi ya mashambulizi na kujizuia.



Meja Jenerali Francis Omondi Ogolla

Kundi la nchi saba tajiri duniani la G7, linalozijumuisha nchi za Uingereza, Marekani, Ufaransa, Ujerumani, Japan na Canada limetoa wito wa kutochochewa kwa mivutano katika eneo hilo.

Rais wa Halmashauri kuu ya Umoja wa Ulaya Ursula von der Leyen, alisema dunia inapaswa kufanya kila linalowezekana ili pande zote zizuie kutanuka kwa mvutano.

"Tunapaswa kufanya kila liwezekanalo ili pande zote zizuie kutanuka kwa mzozo katika eneo hilo. Tumeshuhudia mashambulizi makubwa ya ndege zisizo na rubani na makombora karibu 300 yaliyoendeshwa na Iran dhidi ya Israel. Ni muhimu kabisa eneo hilo libaki kuwa tulivu na kila upande ujiepushe na kuchukua hatua zaidi." Alisema Der Leyen

Nchi ya Australia imewataka raia wake kuondoka haraka Israel na katika maeneo ya Palestina, ikieleza kuna tishio la kutokea mashambulizi ya kulipiza kisasi au hata mashambulizi ya kigaidi.

Aidha, shirika la ndege la FlyDubai limefuta safari zake kuelekea nchini Iran.

Kumekuwa na hofu katika eneo zima la Mashariki ya Kati kutumbukia katika vita kamili. Wiki hii, Rais wa Iran Ebrahim Raisi aliionya Israel kutojibu mashambulizi yoyote katika ardhi yake, huku Katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, akionyesha wasiwasi kuwa eneo la Mashariki ya Kati linakabiliwa na hatari ya vita.

**MAREKANI YAKANA**

Hata hivyo, Marekani imekana kuwa nyuma ya shambulizi hilo la Israel kwa kueleza haikuhusika na mpango wowote.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, alisema kwamba atakuwa amechoka kuzungumzia suala hilo na kukataa kuzungumzia shambulio lililofanywa na Israel dhidi ya Iran.

Blinken alisema kwamba nchi yake haikuhusika katika operesheni yoyote ya kijeshi na inaendelea kufanya juhudi kwa ajili ya kuhakikisha pande mbili zinapunguza kasi ya mgogoro huo.

Wakati akijibu swali la pili kuhusu jinsi gani atakavyoonyesha hali ya mahusiano kati ya Marekani na Israel, Blinken alijibu kuwa wanazungumza mara kwa mara na kila siku kuhusu msimamo wao.

"Tumejitolea kuisaidia Israel kujilinda na kama ni muhimu kushiriki katika utetezi wake, kama ulivyoona siku chache zilizopita." Alisema Blinken

**UN YAONYA**

Katibu nmkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ameonya tabia ya kulipiza visasi na kueleza wakati umefika kwa kukomesha.

Kulingana na taarifa kutoka kwa msemaji wake, ilisema kiongozi huyo aliita tabia hiyo sawa na mzunguko hatari wa kulipiza kisasi katika Mashariki ya Kati.

Guterres aliongeza kuwa analaani kitendo chochote cha kulipiza kisasi na alitoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kufanya kazi kwa pamoja ili kuzuia maendeleo yoyote zaidi yanayoweza kusababisha madhara kwa eneo zima la mashariki ya Kati na sehemu nyingine duniani.

**Mashirika ya kimataifa**



Raia wa Iran akitembea katika mtaa mmoja katika jiji la Tehran nchini Iran baada ya shambulizi lililofanywa na Israel jana. **PICHA: GETTY IMAGES**

## Kenya kuchunguza ajali iliyomuua mkuu wa jeshi

**NAIROBI,** KENYA

SERIKALI ya Kenya imetangaza kuunda timu ya kuchunguza ajali ya helikopta iliyosababisha kifo cha Mkuu wa Jeshi la nchi hiyo, Jenerali Francis Ogolla na makamanda wengine tisa.

Hata hivyo, bado haijafahamika chanzo kilichosababisha ajali hiyo.

Jenerali Ogolla alikuwa miongoni mwa watu 12 waliokuwa ndani ya ndege hiyo ya kijeshi iliyoanguka Alhamisi alasiri muda mfupi baada ya kupaa kaskazini-magharibi mwa nchi hiyo.

Miili ya watu waliofariki ilisafirishwa hadi jijini Nairobi pamoja na majeruhi wawili ambao walipelekwa hospitalini kupatiwa matibabu.

Wakati akitangaza kifo hicho, Rais William Ruto, alisema vifo hivyo vimesababisha huzuni nchi nzima na kutangaza siku za maombolezo ya kitaifa.

**BBC**

# Makonda aagiza ukarabati uwanja wa Sheikh Abeid ukamilike haraka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amewaagiza mafundi wanaoendelea na ukarabati wa uwanja wa Sheikh Amir Abeid wa jijini Arusha, kuongeza bidii kwa kuwa utatumika katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi).

Alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati akikagua maendeleo ya ukarabati huo na mgeni rasmi katika maadhimisho hayo anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Maandalizi hayo yanaongozwa na baadhi ya wajumbe wa kamati ya maandalizi ya kitaifa inayoongozwa na Rais wa Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhokya.

"Maandalizi yanaendelea vizuri, lakini niwaombe mafundi wanaofanya kazi ya ukarabati wa majukwaa na maeneo mengine madogo madogo, muongeze juhudi ili ukarabati huu umalizike kwa wakati kwa kuwa siku zilizobakia ni chache," alisema.

Nyamhokya alimhakikishia Makonda kuwa, maandalizi yote yanaendelea vizuri na kamati zote zilizoundwa zinaendelea na majukumu yake kikamilifu ili yakamilike ndani ya muda uliopangwa.

Alisema maadhimisho hayo ni fursa ya kipekee jijini humo kwa kufanya biashara kutokana na idadi kubwa ya wageni watakahudhuria siku hiyo.

Mpaka sasa wameshawasili watu zaidi ya 2,000 wakiwamo wachezaji wanaoshiriki mashindano mbalimbali. Hoteli nyingi kwa sasa zimejaa kutokana na mkoa huu kuwa kitovu cha utalii," alisema.

Maadhimisho haya ya kitaifa yanafanyika jijini Arusha baada ya kufanyika miaka 22, iliyopita.



Wachuuzi wa samaki wakiwa katika mnada wa soko la samaki la Kimataifa la Magogoni maarufu Feri, jijini Dar es Salaam jana, wakisubiri kitoweo hicho, baada ya kuadimika. Kwa mujibu wa wavuvi, samaki wamekuwa adimu kutokana na hali ya hewa mbaya baharini inayosababishwa na kipindi hiki cha msimu wa mvua. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Msama matatani tuhuma za kutapeli viwanja

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI wa Msama Promotion, Alex Msama, anashikiliwa na Jeshi la Polisi, Kanda Maalum ya Dar Salaam, kwa tuhuma za kutapeli viwanja vinne mali ya Beatrice Mchunguzi vyenye thamani inayokadiriwa kuwa Sh. milioni 800.

Msama alikutwa na tuhuma hizo na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, alipokuwa akisikiliza shauri la Msama na Beatrice lililoitishwa katika ofisi za wizara hiyo jana jijini Dar es Salaam.

Katika video fupi iliyotolewa na moja ya chombo cha habari cha serikali jana ilionesha, Silaa akimwagiza Ofisa wa Jeshi la Polisi, kumchukua Msama na kumpeleka kituo cha Polisi kwa hatua nyingine za kisheria.

"Askari hambebagi pingu?" Alihoji Silaa na askari polisi alijibu, "zipo chini hapo kwenye gari." Na kumwagiza askari wampeleke ziliko pingu hizo huku akiendelea kumhoji askari huyo kama amefika na gari aina ya pickup au linaloendana na hadhi ya Msama.

"Nimekuja na gari yangu tu ya... lakini ipo sawa inamfaa," alieleza ofisa huyo wa Polisi, huku akifuatana na Msama kuelekea lilipo gari hilo.

"Iko sawa! Sawa, hauna Pick up ndiyo nzuri kabisa aipande?" Alihoji Silaa wakati huo Msama na ofisa huyo wakielekea kwenye gari tayari kwa safari ya kwenda kituo cha Polisi kwa hatua zaidi.

Silaa amekuwa na mwendelezo wa ziara za kikazi za kusikiliza kero mbalimbali za migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini kupitia Baraza la Taifa la Ardhi.

# Wataka mikakati, sheria kulinda mikopo asilimia 10 halmashauri

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuandaa sheria, kanuni na mikakati madhubuti kabla ya kurejesha mikopo ya asilimia 10 mapato ya ndani ya halmashauri yasiyolindwa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa na baadhi ya wabunge wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka 2024/25.

Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, alisema wakati serikali inasitisha mikopo hiyo kutokana na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22 kubaini ubadhilifu katika mikopo hiyo, iliahidi kuunda kikosi kazi kufanya uchunguzi na kupeleka ripoti bungeni.

Alisema ripoti hiyo iliyotakiwa kupelekwa kwa wabunge wote ili wapate uelewa wa pamoja lakini haijapelekwa hatimaye kushangaa kuona uamuzi tayari umetolewa na inatarajia kuanza kutolewa bila kuwaondoa hofu juu ya kilichofanya inasitishwa kama kimefanyiwa kazi.

"Tukiangalia muda wa kuanza kwa mikopo hii ni Julai Mosi, 2024 na wakati tunaanza mpango huo mpya kumbe TAMISEMI haijarekebisha sheria wala kanuni na taratibu ambazo tunatarajia zisimamie huu mchakato na kutoa muongozo katika vitu hivi vipya na kutuhakikishia kuwa yaliyotokea awali yatadhibitiwa," alisema Mdee.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwanaisha Ulenge, alisema fedha hizo kabla hazijaanza kutolewa zinatakiwa kuwekewa mkakati maalumu ili kuepusha kujitokeza yale ya awali.

Alisema lengo la mikopo hiyo ni kuleta tija kwa walengwa na kufikia uchumi shindani hivyo lazima ufanyike uhakiki wa makini kupitia maofisa maendeleo ya jamii ambao pia wanatakiwa kuongezwa kutokana na kuwepo idadi ndogo hususani kwenye kata.

Pia alisema kama ilivyo sheria ya utolewaji wa mikopo huyo ni lazima wanufaika wapewe mafunzo juu ya namna ya kufanya matumizi bora ya fedha hizo tofauti na sasa ambapo wanufaika hawapewi elimu hali inayosababisha matumizi mabovu.

"Kumpa fedha bila mafunzo ni sawa na kumpa samaki bila ndoano kwani hatoacha kurejea kukuomba samaki mwingine ilihali angepata ndoano asingerudi tena kuomba samaki," alisema Ulenge.

Ripoti ya CAG imebaini katika tathimini aliyoifanya katika mwaka wa fedha 2022/23 kuwa mamlaka 62 za serikali za mitaa hazikuchangia kikamilifu asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye mfuko kama inavyotakiwa, hivyo kusababisha michango ambayo haikuwasilishwa kiasi cha Sh. bilioni 7.27.

Pia imesema hadi kufikia Juni, 30 2023, wanufaika wa mikopo katika mamlaka za serikali za mitaa 151 walikuwa hawajarejesha mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 79.70.

Katika mapitio ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi, alibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 46 zilikuwa na mikopo isiyorejeshwa ya jumla ya Sh. bilioni 5.70 kutoka kwa vikundi 1,334 vilivyositisha kufanya shughuli zao; na vikundi 851 katika mamlaka za serikali za mitaa 19 vilivyoripotiwa kupokea mikopo ya jumla ya Sh. bilioni 2.6 havikuthibitika uwapo wake.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-9

**Na Adam Fungamwangaza**
**(0716 350534)**

Ujumbe huu ulionekana kuwagusa waandishi wa kutaka kujua ni kitu gani ambacho kitafanyika kama ikionekana aliuawa.

"Wamesema vyovyote itakavyokuwa, kama ameuawa, basi damu ya marehemu haitoenda bure. Damu ya Mariamu itawalilia wote waliomuua. Damu ya Mariamu haitokauka ardhini. Damu ya Mariamu itaendelea kumiminika kama chemchem, mpaka pale wote waliohusika wanapatikana na kupata kinachowastahili.

Wazee wamesema wao hawatomaliza msiba huu mpaka wale wote waliofanya hivyo wafahamike na kupata adhabu yao hapa hapa duniani. Hapo ndipo watamaliza msiba, na watajua kuwa ndugu yao sasa amefurahi na kulala kwa amani. Nadhani Jeshi la Polisi ambalo lina nia ya dhati kwa wananchi wake litafanya kama tulivyoagiza. Vinginevyo familia itamshtakia Mungu.

*************************

Polisi wa uchunguzi waliopewa kazi ya kurudia kuchunguza upya walikuja na majibu tofauti na ya awali.

Mwanzo ilisemekana kuwa marehemu alianguka wakati anafanya mazoezi na kwa mujibu wa uchunguzi wa madaktari ni kwamba alipatwa na mshtuko wa moyo.

Safari hii walikiri kuwa ni kweli marehemu aliawa. Taarifa ilisema kuwa aliuawa nyumbani kwake kwa kupigwa na kitu kizito kichwani.

Muuaji alimuua na kumvisha nguo za michezo, 'trakisuti,' kabla ya kwenda kumtupa kwenye mtaro.

Lengo ni kupoteza ushahidi na kuufanya upelelezi kuwa mgumu. Uchunguzi huu ulikuja na mshukiwa wa mauaji hayo. Hakuwa mwingine ila ni Kamal, mchumba wa marehemu.

"Mchumba wa marehemu ndiyo mshukiwa mkuu kwa mujibu wa uchunguzi wa pili uliofanyika, na Jeshi la Polisi linamsaka, na akitiwa nguvuni anatarajiwa kufikishwa kizimbani kwa mauaji, huku upelelezi na ushahidi mwingine ukizidi kukusanywa," lilisema Jeshi la Polisi.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Kamal aliimua mchumba wake kutokana na wivu wa kimapenzi, na sasa hajulikani alipo.

Habari ya Kamal kumuua mchumba wake na kuitupa maiti yake kwenye mtaro ndiyo ilikuwa kuu kwenye vichwa vya habari kwenye magazeti siku hiyo pamoja na mitandao ya kijamii.




**Awali, Kamal aliwaambia ndugu za marehemu kuwa alipoingia ndani katika pekua-pekua aliikuta simu ya Mariamu ndani.**

Ushahidi uliowekwa wazi tu kuwa mtu wa mwisho kuwasiliana na marehemu ni mpenzi wake huyo ambaye alimtaarifu kuwa anakwenda kukagua na kufunga maduka na saluni zake.

Kwa mujibu wake mwenyewe Kamal kuwa aliongea na Mariamu, lakini simu ilikuwa haipatikani. Na haikupatikana tena hadi mwenye simu alipokutwa akiwa maiti.

Kwa mujibu wa upelelezi ni kwamba baada ya kuongea naye akamwambia amsubiri nyumbani ili watoke naye.

Kamal yeye alisema aliamua kumfuata Mariamu na bodaboda saa sita usiku baada ya kuona simu haiiti kwa muda mrefu, kitu ambacho si kweli, badala yake muda ule ule tu wa saa 1:00 usiku alikwenda kwa mpenzi wake.

Alisema alipofika hakumkuta mpenzi wake, badala yake akafungua mlango kwa fungo nyingine ambazo anazo, lakini kwa mujibu wa uchunguzi wa polisi ni kwamba alimkuta na akafanya alivyofanya, ambapo ni kumuua, kisha akaichukua maiti na kwenda kuitupa kwenye mtaro, na baada ya hapo akaanza kupigia simu ndugu zake kuwa mpenzi wake hapatikani kwenye simu.

Awali, Kamal aliwaambia ndugu za marehemu kuwa alipoingia ndani katika pekuapekua aliikuta simu ya Mariamu ndani.

Ukweli kwa mujibu wa uchunguzi ni kwamba, baada ya kumuua mpenzi wake, aliizima simu ili asipigiwe simu na mtu yoyote kwa sababu iwapo ingekuwa haipokelewi, wengi wakiwemo rafiki na ndugu wangepatwa na wasiwasi na kumtafuta.

"Uchunguzi huu tunamtuhumu mchumba wake Kamal kuwa amehusika, na hii ni kwa sababu Mariamu amekuwa akitakiwa na wanaume wengi, na ushahidi unasema Kamal amekuwa anakuta meseji nyingi kwenye simu ya marehemu alizotumiwa na wanaume wengine, wivu ulimfanya kushikwa na hasira na kutekeleza mauaji hayo ambayo aliyapanga kwa uangalifu ili asikamatwe."Msemaji wa Jeshi la Polisi alitanabaisha.

Ndugu wa marehemu sasa waliridhika uchunguzi wa pili, wakakubali kuchukua mwili wa marehemu kwenda kuuzika kwenye makaburi ya Chang'ombe, Dar es Salaam.

Mazishi hayo yalihuduriwa na watu wengi, kasoro mtu mmoja tu hakuwepo. Ni Kamal. hakuwepo kwa sababu anatafutwa kwa udi na uvumba na polisi kwa sasa yeye ndiyo aliyefanya mauaji hayo.

Alikokimbilia hakujulikani, lakini polisi waliahidi kufanya msako kabambe na kumpata popote pale, hata kama atakuwa amekimbilia nje ya nchi, basi watatumia polisi wa kimataifa, 'Interpol' ili kumkamata na kurejesha nchini aje kujibu mashtaka, ambapo kama ikithibitika adhabu yake ni kunyongwa hadi kufa.

***************************

Alikuwa ndani ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, akiangalia moja kati ya mechi ambazo timu anayoipenda, Simba.

Simu ilipigwa lakini kutokana na makelele ya uwanjani hakuisikia. Mechi ilipomalizika, aliingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake kwa sababu kuna mtu alitaka kumpigia.

Alikutana na 'miss call', sita, za mtu ambaye anamfahamu. Ni mmoja wa ndugu wa Mariamu. Ataitwa Teddy. Undugu wao ni kwamba mmoja alizaliwa kwa mama mkubwa, mwingine mdogo. Alifanana sana na marehemu Mariamu. Kutokana na kufanana huko, Kamal alikuwa anapenda mno kumtania. Alimwita mke mdogo. Mariamu alizaliwa na mkubwa, Teddy mdogo, ambapo mama zao walizaliwa tumbo moja.

Kamal alimzoea zaidi Teddy kuliko ndugu wengine. "Yaani mmefanana na dada yako kama korosho." Kamal alikuwa akimtania Teddy.

"Ikitokea bahati mbaya nikifa, muoe Teddy, mimi nitakuwa radhi kabisa, lakini ukiona mwanamke mwingine nitakutokea usiku wewe na huyo mkeo." Ni maneno aliyokuwa akiyaongea Mariamu mara kwa mara, anapokuwa na Kamal pamoja na Teddy.

Hakuna aliyekuwa akiyatilia maanani kwa sababu yalionekana ni kama maneno ya utani na kunogesha stori.

"Dada aliyekwambia wewe utaanza kufa kabla ya mimi nani? Ushaanza hivyo, hapa tuko kwenye furaha unaanza mambo yako." Teddy huwa wanajibu.

"Nasema ikitokea, sisi binadamu, huoni tulivyofanana, Kamal akiwa na wewe ataona kama yupo na mimi tu."

"Teddy, achana na dada yako, anatuvuruga tu hapa, ukiolewa je, halafu ikitokea yeye amekufa na wewe upo kwenye ndoa, nitaachanisha ili nimuoe?"

Hayo ni maongezi ya mara kwa mara ambayo huongelewa pale, Kamal anapokuwa pamoja na ndugu hao wawili, Mariamu na Teddy, ambapo huwachukua na kwenda nao kula bata, mwenyewe anawaita wake zake, Mariamu mkubwa, Teddy mdogo.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KMC YAONGOZA KWA SARE LALA SALAMA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya KMC ya Dar es Salaam inaongoza kwa kupata idadi kubwa ya matokeo ya sare katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaelekea ukingoni.

Timu hiyo inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni, imetoa sare katika michezo yake 11, ikiwa ni wastani ya nusu ya mechi zote ilizocheza mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo la Nipashe na za Bodi ya Ligi, KMC inayokamata nafasi ya tano mpaka sasa ikiwa na pointi 32 kibindoni, imecheza mechi 23, ikishinda michezo saba na kupoteza mitano.

Timu zinazofuatiwa na kutoa sare nyingi ni Kagera Sugar, JKT Tanzania na Tabora United, ambazo zote zimetoa sare mara 10 kila moja mpaka sasa.

**Mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Yanga, ndiyo timu iliyotoa sare chache zaidi, ikifanya hivyo mara moja tu, ambayo iliipata Februari 2, mwaka jana walipocheza kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani, Kagera dhidi ya wenyeji.**

Katika mechi hiyo, Kagera Sugar iliibana Yanga na dakika 90 ziliponmalizika, matokeo yalikuwa ni suluhu.

Mtibwa Sugar ambayo sasa iko chini ya kiungo wake wa zamani, Zuberi Katwila, imepoteza idadi ya mechi nyingi katika ligi mpaka sasa, ikipigwa michezo 13, ikifuatiwa na Mashujaa FC, ambayo imepoteza mechi 11, huku timu za Simba, Yanga na Azam zikipoteza mara chache zaidi, kila timu ikifungwa mara mbili.

Wakati Yanga ikiwa ndiyo timu yenye mabao mengi zaidi, ikipachika mabao 52 kabla ya mechi ya leo dhidi ya Simba, Dodoma Jiji, Geita Gold, JKT Tanzania na Tabora United zimefunga mabao machache zaidi, kila moja ikipachika magoli 16 tu, zikizidiwa na hata Mtibwa Sugar inayoshikilia mkia, lakini yenyewe imefunga mabao 22.

Pamoja na kuwazidi wenzake katika mabao ya kufunga, Mtibwa Sugar, ndiyo timu iliyopachikwa mabao mengi zaidi mpaka sasa, ikiruhusu mabao 37, wakati Yanga ni timu iliyoruhusu mabao machache zaidi katika nyavu wake kabla ya mechi ya leo, ikiwa imefungwa mabao 11 tu.

Timu tatu ambazo ziko katika hatari ya kushuka daraja ni pamoja na JKT Tanzania ya Dar es Salaam, Mashujaa kutoka Kigoma na Tabora United ya mkoani Tabora ambayo inatumia Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

# Ali Hassan Mwinyi yapigiwa debe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa serikali inajenga na kukarabati viwanja vitakavyotumika katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika nchini ifikapo mwaka 2027 (AFCON 2027).

Viwanja hivyo ni pamoja na Benjamin Mkapa kilichopo Dar es Salaam, Amaan (Zanzibar) na Uwanja mpya wa Samia unaojengwa jijini, Arusha.

**Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Hawa Mwaifunga.**

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itafanya ukarabati mkubwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi ulioko Tabora ili pia utumike katika fainali za AFCON 2027.

Akijibu swali hilo, alisema serikali inatambua umuhimu wa ukarabati wa uwanja wa mpira wa Ali Hassan Mwinyi uliopo Tabora pamoja na viwanja vingine hapa nchini.

"Serikali imeendelea kusisitiza wadau na wamiliki wa viwanja kujenga na kutunza miundo mbinu hiyo sawa na maelekezo ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995, sehemu ya 7 (i) - (vi)," alisema.



Kipa wa Pamba FC ya jijini, Mwanza, Shabani Kado, akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya TMA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha. **PICHA: MTANDAO**

# KMKM, KVZ zatinga robo fainali ZFF Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za KVZ na KMKM zimefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la ZFF (FA CUP) baada ya kufanya vizuri katika michezo yao ya hatua ya 16 bora.

KVZ imesonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuifunga Raskazone mabao 3-1 wakati KMKM wameichapa Paje Star magoli 4-1, michezo yote imechezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi jioni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KVZ, Ali Mohamed Ameir, alisema licha ya timu yake kutocheza vizuri katika mchezo wao dhidi ya Raskazone FC lakini anafurahi kuona wamefanikiwa kutimiza malengo yao kwa kutinga hatua ya robo fainali.

Ameir alisema kupitia mchezo huo ameona mapungufu ya wachezaji wake ikiwamo la kukosa ‚fitness', hivyo ataenda kulifanyia kazi kabla ya kuanza kwa michezo ya Ligi Kuu Zanzibar.

"Tumetoka na ushindi, lakini bado sijaridhishwa na viwango vya baadhi wa wachezaji wangu, hawana fitness hali iliyopelekea kukosa nafasi nyingi sana za kufunga, na hii imetokana bado wanauchovu wa mapumziko ya mwezi mzima," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema mchezo huo ulikuwa mgumu kwa sababu uliwakutanisha na wachezaji vijana wanaoshiriki Ligi ya Kanda, Paje Star FC ambao miili yao bado ina nguvu, kasi na inatamani kucheza mpira.

Msimu alisema wapinzani wake walicheza vizuri lakini walikosa uzoefu na mbinu za kiufundi jambo ambalo KMKM liliwapa faina na kuondoka na ushindi.

Alisema baada ya kuvuka hatua hiyo ya 16 bora sasa wanaendelea na kampeni yao ya kuhakikisha wanatwaa taji la ubingwa wa michuano hiyo kwa msimu huu.

"Kadri tunavyosonga mbele ndio tunajiandaa zaidi katika hizi mbio zetu za kuutaka ubingwa wa FA, tunaimani kubwa katika hatua ya robo tutafanikiwa kusonga mbele," Msimu aliongeza.

Mechi za hatua ya 16 bora zitaendelea tena leo kwa Kundemba kukutana na Taifa Jang'ombe kwenye Uwanja wa Mau A wakati Maafande wa JKU wataikaribisha Nyangobo FC kwenye Uwanja wa Mau B , michezo yote itachezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Bingwa wa michuano hiyo atapata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika yaliyoko chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

## ZISIKUPITE

### CITY YAMTAKA MUSIALA

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Jamal Musiala, ameibuka kama shabaha kuu ya Manchester City msimu wa joto, huku Chelsea pia wakifuatilia hali ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani. (***Guardian***)

### OLISE ANUKIA ARSENAL

KLABU ya Arsenal inatazamia kumsajili mshambuliaji na winga katika msimu wa joto, huku mshambuliaji wa Newcastle United, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 24, na winga wa Ufaransa, Michael Olise mwenye miaka 22, ambaye yuko Crystal Palace, wakiwa miongoni mwa malengo yao. (***Guardian***)

### ARSENAL YAMWINDA SESKO

ARSENAL inamfuatilia mshambuliaji wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko, mwenye umri wa miaka 20 huku wakiongeza juhudi za kusajili mshambuliaji msimu huu. (***Standard***)

### CHELSEA, UNITED VITANI

CHELSEA na Manchester United pia zinamfuatilia mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Slovenia, Benjamin Sesko, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 50. (***Ben Jacobs***)

### LIJNDERS SOKONI UTURUKI

KOCHA Msaidizi wa Liverpool, Pep Lijnders, ananyatiwa na Besiktas kwa ajili ya kuchukua nafasi ya kocha mkuu wa timu hiyo ya Uturuki iliyopo wazi. (***Athletic***)

### PSG YAMTAJA COLWILL

LIVERPOOL na Paris St-Germain zinafikiria kumnunua mlinzi wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Levi Colwill, mwenye umri wa miaka 21. (***GiveMeSport***)

### GNABRY AKARIBIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Serge Gnabry, huku Bayern Munich wakiwa tayari kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 28. (***Football Insider***)

### GIBBS-WHITE KUTUA SPURS

TOTTENHAM Hotspur pia inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumwania kiungo wa Nottingham Forest, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 24, na wako tayari kumnunua msimu wa joto. (***Football Insider***)

### LUKAKU KUREJEA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, anatarajiwa kurejea Chelsea mwishoni mwa msimu wake wa mkopo wa muda mrefu akitokea AS Roma, ambayo haiwezi kumudu euro milioni 43 kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 30 kwa mkataba wa kudumu. (***Gazzetta dello Sport***)

### RAMSDALE ATAJWA NEWCASTLE

CHELSEA na Newcastle United zinavutiwa na mlinda lango wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Aaron Ramsdale, mwenye umri wa miaka 25. (***CaughtOffside***)

### NAGELSMANN AFUNGUKA

KOCHA wa Ujerumani, Julian Nagelsmann, haongeitu na Bayern Munich kuhusu kuwa kocha wao na atafanya uamuzi ndani ya wiki ijayo au zaidi, kwa mujibu wa wakala wake. (***Metro***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: TUTASAJILI MSHAMBULIAJI MPYA

### ●●● Toney, Gyokeres, Sesko watajwa katika rada za klabu...

**LONDON,** England

ARSENAL inaongeza kasi ya kutafuta angalau mshambuliaji mmoja mpya baada ya wiki hii kuondolewa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich, vyanzo vimeiambia ESPN.

Jaribio la Arsenal la kutinga hatua ya nusu fainali ya kwanza tangu mwaka 2009 liliisha kwenye Uwanja wa Allianz Arena juzi usiku huku Joshua Kimmich akifunga kwa kichwa dakika ya 63 na kuwapa ushindi wa jumla wa mabao 3-2 kwa wababe hao wa Bundesliga.

Vyanzo vimeiambia ESPN klabu hiyo sasa imeweka nguvu kujiimarisha katika nafasi kadhaa lakini inaipa kipaumbele katika kuimarisha safu yao ya mbele, kwa kutafuta mshambuliaji na winga.

Kai Havertz ametumika kama mshambuliaji wa kati katika wiki za hivi karibuni huku Gabriel Jesus akipewa jukumu kubwa na Eddie Nketiah hajaanza mchezo wowote katika mashindano yoyote tangu Arsenal ilipofungwa mabao 2-1 na Fulham usiku wa kuamkia mwaka mpya.

Kwa muda mrefu Arsenal walikuwa na nia ya kutaka kumsajili mchezaji wa Brentford, Ivan Toney, lakini vyanzo vya ndani vimesema kwa sasa wanaangalia chaguzi nyingine.

Vyanzo vya nje ya Arsenal vimeiambia ESPN miongoni mwa wachezaji wanaozingatiwa ni mshambuliaji wa Sporting Lisbon, Viktor Gyökeres, ambaye alihamia Ureno kutoka Coventry City msimu uliopita, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ana mabao 36 na asisti 16 katika mechi 44 msimu huu.

Mchezaji wa RB Leipzig, Benjamin Sesko ni mshambuliaji mwingine chipukizi ambaye Arsenal wamewahi kumsaka mara kadhaa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 ana kifungu cha kutolewa cha euro milioni 50 ambacho kitaanza kutumika msimu huu wa joto. Arsenal pia imekuwa ikimfuatilia winga wa Wolves, Pedro Neto, kwa muda mrefu.

Arteta alidokeza mipango ya klabu hiyo mapema mwezi huu alipofichua angependa kufanya kazi na kikosi kidogo lakini chenye ubora wa juu ili kuongeza mzunguko, sawa na Manchester City ya Pep Guardiola.

„Ningependa hiyo, kuwa na wachezaji 22 au 20 badala ya 18," alisema Arteta mapema mwezi huu.

HABARI MICHEZO

# LIVERPOOL SASA NGUVU ZOTE LIGI KUU ENGLAND



**LIVERPOOL,** England

KUONDOLEWA kwa Liverpool katika robo fainali ya Ligi ya Europa kutawasaidia kuelekeza nguvu zao katika kutafuta ubingwa wa Ligi Kuu England, Kocha Jurgen Klopp, amesema.

Walifungwa mabao 3-0 na Atalanta katika mechi ya kwanza kwenye Uwanja wa Anfield, na penalti ya mapema ya Mohamed Salah katika mechi ya marudiano iliyochezwa juzi iliipa Liverpool ushindi wa ugenini wa goli 1-0, lakini vijana wa Klopp walitolewa kwa jumla ya 3-1.

„Tumesikitishwa hatukupita lakini hatukuchanganyikiwa au kukasirika. Sasa tunaweza kujikita zaidi kwenye ligi na hilo ndilo tutafanya," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

„Tuna siku chache za kupona halafu tutacheza na Fulham, jambo ambalo litakuwa gumu lakini tutatoa kila kitu. Hayo ndiyo mashindano yetu sasa."

Liverpool walio nafasi ya tatu wako sawa na Arsenal wakijikusanyia pointi 71 lakini wamepitwa mabao, huku viongozi Manchester City wakiwa na pointi 73.

Klopp alisema hakujali kuhusu kiwango cha Salah alipoulizwa kuhusu uchezaji wa fowadi huyo katika michezo ya hivi karibuni.

„Penati hiyo ilikuwa ya kustaajabisha, penalti ya hali ya juu, halafu nafasi iliyofuata, hiyo haikuwa bahati lakini si mara ya kwanza kukosa nafasi kama hiyo," aliongeza Klopp.

## Martinez aibuka shujaa Ufaransa



**LILLE,** Ufaransa

MSHINDI wa Kombe la Dunia, Emiliano Martínez, alizalisha ushujaa zaidi wa penalti, akiokoa mara mbili na kuisaidia Aston Villa kuifunga Lille 4-3 na kutinga nusu fainali ya Ligi ya Europa Conference, hapo juzi.

Martínez aliokoa penalti ya Nabil Bentaleb na ule wa mwisho wa Benjamin André, na kuiwezesha Villa kusonga mbele.

Martínez alikuwa anazomewa wakati wote wa mchezo huo na mashabiki wa Lille, kutokana na vitendo vyake vilivyomfanya katika mechi ya fainali ya Kombe la Dunia ya mwaka 2022.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 aliokoa penalti moja ya Ufaransa na pia akapata kadi ya njano kwa majaribio lake la kuwavuruga wapinzani huku Argentina ikinyanyua kombe hilo kwa mara ya tatu nchini Qatar, na kujipatia hadhi ya shujaa wa Argentina na nafasi ya mhalifu wa Ufaransa.

„Yeye ni muhimu sana kwetu," alisema Kocha wa Aston Villa, Unai Emery, kuhusu kipa wake.

"Ana utu wake katika chumba cha kubadilishia nguo ni muhimu sana kwa sababu ni kiongozi mwenye uzoefu wake.

„Ana akili nzuri sana. Na halafu uwanjani ana haiba yake na alicheza vizuri. Aliokoa michomo miwili ya penalti kwa hivyo bila shaka ninajivunia sana. Ninajivunia sana wachezaji wote."

Baada ya ushindi wa 2-1 katika mkondo wa kwanza wa robo fainali wiki iliyopita, Lille ilionekana kutinga hatua ya nne bora wakati mabao kutoka kwa Yusuf Yazici na André katika kila kipindi kuwaweka mbele kwa jumla ya 3-2.

Lakini Matty Cash aliisawazishia Villa zikiwa zimesalia dakika tatu za muda wa kawaida.

## Nagelsmann ageuka lulu Ulaya

**MUNICH,** Ujerumani

WAKALA wa Julian Nagelsmann amethibitisha mazungumzo yanafanyika na klabu nyingi zaidi ya Bayern Munich huku kocha huyo mkuu wa sasa wa Ujerumani akifikiria uhamisho wake mwingine.

Kocha huyo wa zamani wa Bayern Munich, ambaye alitimuliwa kwa mshangao na wababe hao wa Bavaria miezi 13 tu iliyopita, ana mkataba na Chama cha Soka cha Ujerumani (DFB), hadi mwisho wa Euro 2024 kwenye ardhi ya nyumbani msimu huu wa joto.

Wakati huo, anatazamiwa kurejea katika soka ya klabu, baada ya kujitambulisha kama kocha kijana akiwa hajatimiza umri wa miaka 30.

Akimwakilisha Nagelsmann, Volker Struth alisema uamuzi kuhusu mustakabali wa kocha huyo mwenye umri wa miaka 36 huenda ukafanywa haraka sana.

„Itaamuliwa hivi karibuni, katika siku tano, sita au saba zijazo. Itakuwa upuuzi mtupu kusema hatuzungumzi na wahusika," aliongeza Struth.

„Bila kusema wahusika ni akina nani, naweza kusema sio tu Bayern Munich. Hiyo ni kawaida. Ni kazi yangu na itakuwa mzaha kidogo kwenye vyombo vya habari kusema hatuko kwenye mazungumzo," alifafanua.

Bayern Munich wanamwinda kocha mpya baada ya tayari kuthibitisha, Thomas Tuchel, ambaye alichukua nafasi ya Nagelsmann, ataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto.



# MABINGWA MTOKO WA KIBINGWA WATUA, WAMTAJA AZIZ KI, CHAMA

Mwandishi Wetu

WAKATI mashabiki wakihesabu saa chache ili kufanyika mechi ya marudiano ya watani wa jadi, Simba na Yanga katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu itakayochezwa leo, mabingwa wa Mtoko wa Kibingwa wamewasili Dar es Salaam tayari kuishuhudia dabi hiyo.

Mabingwa hao ambao ni washindi wa kampeni ya Mtoko wa Kibingwa iliyotoa fursa kwa mashabiki 56 kuishuhudia dabi hiyo kwa hadhi ya VIP kwa gharama za Betika, wamewasili jijini na kuwataja nyota wa timu hizo, Stephanie Aziz Ki wa Yanga na Clatous Chama wa Simba ndio wanawatarajia kuamua mechi hiyo.

Wengi wao kutoka nje ya Dar es Salaam wamesema, hii ndiyo mara yao ya kwanza kuishuhudia dabi hiyo ‚laivu', na hata kusafiri kwa ndege.

„Betika waliponipigia simu nilikuwa shambani, sikuamini, nilihisi ni utani, ila nikasema ngoja niende nao hadi mwisho nione itajavyokuwa," alisema Uria Mtalika wa Kaliua mkoani, Tabora.

Shabiki huyo kindaki ndaki wa Yanga alisema, Jumatano iliyopita alitoka Kaliua hadi Tabora mjini kama alivyoelekezwa na mwakilishi wa Betika.

„Niliendelea kuwasiliana nao, lakini sikuwa naamini hadi nilipopanda ndege na leo (jana) nipo Dar nikisubiri kuishuhudia dabi," alisema Mtalika huku akiitabiria timu yake ushindi wa mabao 2-0.

Mshindi mwingine, Kimara Mapunda kutoka Sumbawanga aliliambia gazeti hili mechi ya leo roho yake ipo kwa Simba.

„Nawashukuru Betika kwa kuweka fursa ya Mtoko wa Kibingwa, nilicheza bila kukata tamaa hadi nimeshinda na kuja kutizama dabi, hii ni mara yangu ya kwanza kushuhudia dabi, kinachonivutia zaidi ni kuja kuwaona wachezaji wa Simba hasa Chama na Kibu Denis, nawakubali sana," alisema.

Naye shabiki wa Simba, Mussa John, wa Arusha alisema anaamini watalipa kisasi leo kwa kuichapa Yanga mabao matano huku Clinton Festo wa Kigoma alisema hana shaka na timu yake kupata matokeo, lakini Aziz Ki na Pacome anaamini wataiduwaza Simba.

Akizungumza mara baada ya kuwapokea mabingwa hao, Balozi wa kampeni hiyo msimu huu, Baraka Mpenja, alisema mashabiki wote wataishuhudia dabi kwa hadhi ya VIP.

„Hawa wa mikoani wataungana na mabingwa wetu wa Dar es Salaam ambao leo (jana) watalala kwenye hoteli ya nyota tano kabla ya kwenda uwanjani wakiongozwa na king'ora kushuhidia dabi hiyo wakiwa kwenye jukwaa la VIP," alisema Mpenja.

Mbali na mabingwa, Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa, alisema kulikuwa na zawadi mbalimbali za wiki na mwezi kwenye kampeni hiyo.

„Kila wiki tulikuwa na washindi wa simu janja aina ya tecno na kila mwezi tulikuwa na washindi wawili wa iphone 15 ili kunogesha kampeni yetu hadi leo (jana) tumewapokea mabingwa wetu.

„Betika ni bandika bandua, hatuna mbambamba, baada ya dabi, mashabiki wetu wakae mkao wa kitu kingine bomba," alisema Rugambwa.

## Dabo auchambua ubingwa Ligi Kuu

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amekiri kuwapo kwa ugumu wa Ligi Kuu Tanzania Bara hususani mzunguko wa pili ambao kila timu inahitaji ushindi ili kufikia malengo yao.

Dabo aliliambia gazeti hili kwa upande wao wanahitaji alama muhimu kwa kila mechi watakayocheza kwa lengo la kujihakikishia wanamaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ili kupata tiketi ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha huyo alisema mikakati yake ni kuona timu yake inafikia malengo ambayo waliyaweka tangu mwanzoni mwa msimu na watapambana ili kufikia ndoto zao.

"Sio rahisi kushinda mechi zote, tunauwezo wa kumfunga kila mpinzani anayekuja mbele yetu, lakini kuna wakati mwingine tukubali hatuwezi kushinda kwa kila mechi. Tunahitaji umakini zaidi katika mechi zetu zijazo kwa sababu hakuna mchezo utakaouwa rahisi," alisema kocha huyo.

Aliongeza anaandaa kikosi imara kwa kuwapa mbinu za kiufundi mbalimbali na kuwaweka sawa kisaikolojia kutokana na ushindani uliopo kwenye hatua hii ya lala salama.

Dabo alisema pia malengo yake mengine ni kufanya vyema katika mchezo wao wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho la CRBD Bank dhidi ya Namungo utakaochezwa kati ya Mei 2 na 4, mwaka huu.




Balozi wa Kampuni ya Betika, Baraka Mpenja (mwenye suruali ya kaki), akiwa na baadhi ya washindi wa Mtoko wa Kibingwa baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam tayari kuishuhudia dabi ya Simba na Yanga itakayochezwa leo. **MPIGAPICHA WETU**

## Dabi 6 zisizosahaulika

INATOKA UK. 24

wa na Jumanne Hassan ‚Masimanti' na beki, Selemani Sanga wa Yanga akijifunga mwenyewe.

**3. Simba 4-4 Yanga (1996)**

Mechi hii inabaki katika vitabu vya kumbukumbu kuwa ndiyo sare iliyozaa mabao mengi zaidi kwenye mchezo wa dabi.

Mechi ilichezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha, mabao ya Yanga yakifungwa na Edibily Lunyamila, Mustapha Hozza (akijifunga), Said Mwamba ‚Kizota' na Sanifu Lazaro, huku ya Simba yakipachikwa na Thomas Kipese, Ahmed Mwinyimkuu na Dua Said akipiga mawili.

**4. Simba 5-0 Yanga (2011/12)**

Ni moja kati ya mechi za kukumbukwa za watani wa jadi, ikichezwa Mei 6, mwaka 2012, Simba ilipata matokeo hayo kupitia mabao yaliyowekwa kimiani na Emmanuel Okwi, aliyefunga mawili, Felix Sunzu, Patrick Mafisango (marehemu) na Juma Kaseja, wote wakifunga magoli hayo kwa penalti.

**5. Simba 3-3 Yanga (2013/14)**

Ilikuwa ni moja kati ya dabi za kushangaza ambapo hadi mapumziko Yanga ilikuwa ikiongoza mabao 3-0, lakini Simba ikarudisha magoli yote kipindi cha pili.

Dabi hiyo ilichezwa Oktoba 20, mwaka 2013, Yanga ikitangulia kwa mabao ya Mrisho Ngassa na Hamisi Kiiza wakati Simba ilisawazisha kupitia Betram Mombeki, Joseph Owino na Gilbert Kaze.

**6. Yanga 5-1 Simba (2023/24)**

Hii ni dabi ya mzunguko wa kwanza msimu huu, ambapo Yanga ilitoa kipigo kikubwa cha mabao 5-1, mechi iliyochezwa Novemba 5, mwaka jana.

Yalikuwa ni mabao ya Kennedy Musonda, Maxi Nzengeli (mawili), Stephane Aziz Ki na Pacome Zouzoua.

# Simba, Yanga na safari ya ubingwa

INATOKA UK. 24

mchezo mkubwa kwa Afrika.

Gamondi alisema wamejiandaa vizuri kama kawaida, wachezaji wake wana morali nzuri na wapo tayari kukabiliana na mpinzani wao, Simba katika mchezo wa leo.

"Kesho (leo) ni mechi nyingine na mipango yake ni mingine, huu mchezo ni tofauti na ule uliopita, tutacheza kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunafanikiwa kupata matokeo chanya," alisema Gamondi.

Beki wa Yanga, Dickson Job, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kupambana kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya mbele ya mpinzani wao.

"Simba ni timu nzuri na hautakuwa mchezo rahisi, mchezo utakuwa mgumu, kikubwa tunahitaji pointi tatu, hatuchezi kwa presha kubwa wala matokeo ya kutaka kushinda mabao mengi kikubwa ni alama muhimu," alisema Job.

Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, alisema maandalizi yanaenda vizuri na siku zote hakuna mechi rahisi ya dabi na anawaheshimu Yanga.

"Hatuna presha kabisa, mechi ya dabi ni tofauti kabisa na michezo mingine, tumefanya maandalizi mazuri kukabiliana na Yanga, Kocha Abdelhak (Benchikha), anaumia sana pale tunapotengeneza nafasi na haziwi mabao, tumeliangalia na kufanyia kazi, nafasi zinazopatikana ziwe mabao.

Mbio za ubingwa zipo wazi na mchezo wa kesho (leo), ndio unatoa taswira ya nani kubwa bingwa, tukihitaji ubingwa lazima tushinde mechi ya kesho (leo) dhidi ya Yanga," alisema Matola.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Shomari Kapombe, alisema maandalizi yameenda vizuri na wachezaji wana morali kubwa kwa ajili ya mchezo wa leo huku benchi la ufundi likipata muda mzuri wa kuandaa timu yake.

Kapombe alisema wapo tayari kufuata maelekezo waliyopewa na kila mmoja kufanya jukumu lake kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu.

„Kwa sasa hatufikirii mechi iliyopita, tumefungua ukurasa mpya na hii mechi ni aina nyingine, tumekuwa na mikakati mipya kuhakikisha tunavuna pointi tatu," alisema Kapombe.

Aliongeza mechi ya leo itakuwa ni hatima ya malengo ya kusaka tiketi yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na anaimani hadi sasa bado hajajulikana bingwa hadi mwisho wa msimu.

# Michezo

Jumamosi Aprili 20, 2024

Nipashe



Nagelsmann ageuka lulu Ulaya UK. 22

# SIMBA SC, YANGA NA SAFARI YA UBINGWA

**Na Saada Akida**

## ●●● Mechi ya leo inatarajia kutoa mwelekeo katika mbio za kuwania taji la...

ZIKIWA na kumbukumbu ya kuishia katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa vigogo wa soka nchini, Yanga na Simba watakutana katika mechi ya dabi itakayochezwa leo kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo ni ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara na wenyeji wa mchezo huo, Yanga wataingia dimbani na kumbukumbu ya ushindi mnono wa mabao 5-1, ambayo yalifungwa na Stephane Aziz Ki, Pacome Zouzoua, Kennedy Musonda na Maxi Nzengeli aliyefunga mawili.

Bao pekee la Simba katika mchezo huo lilifungwa na Kibu Denis.

Katika rekodi zetu kuanzia mwaka 2010, zinaonyesha Aprili timu hizo zimekutana mara nne, Simba walifanikiwa kushinda mara mbili na michezo mingine miwili iliyobakia ilimalizika kwa matokeo ya sare.

Aprili 18, 2010 Simba alishinda mabao 4 -3, na mabao yake yalifungwa na Uhuru Suleiman dakika 3, Mussa Mgosi (dk 53 na dk 74), Hillary Echesa (dakika za nyongeza) huku kwa upande wa Yanga yalipachikwa na Athumani Iddi ‚Chuji' dakika 30 na Jerry Tegete aliyefunga mawili (dakika 69 na 89).

Mechi ya kwanza ya Aprili 19, 2014 iliisha kwa sare ya bao 1-1, Simba walitangulia kupata bao kupitia Haruna Chanongo na dakika nne kabla ya mechi kumalizika, Yanga walisawazisha kupitia Simon Msuva.

Msimu wa 2017/18 mechi iliyochezwa Aprili 20, Simba walifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0, kupitia Erasto Nyoni na timu hizo ziliporudiana mchezo ulimalizika kwa suluhu.

Mchezo wa mwisho uliochezwa Aprili 16, mwaka jana, Simba iliondoka na pointi tatu baada ya kushinda mabao 2-0, shukrani beki Henock Inonga akipachika bao la mapema dakika ya kwanza na lingine lilifungwa na Kibu Denis dakika 32.

Mechi ya leo haitakuwa ya kinyonge kutokana na rekodi za timu hizo hivi karibuni, mechi tano za mwisho walizokutana Simba ilishinda mbili na Yanga mara moja, wakitoka sare mara mbili.

Yanga inashuka dimbani ikiwa na safu imara ya ushambuliaji inayoongozwa na Stephane Aziz Ki ambaye ametikisa nyavu mara 14 pamoja na Nzengeli aliyefunga magoli tisa wakati Simba inamtegemea Clatous Chama mwenye magoli saba sawa Mrundi Saido Ntibazonkiza.

Yanga na Simba, zote zipo katika mbio za ubingwa, Yanga wakiongoza kwenye msimamo baada ya kujikusanyia pointi 55 na Simba iliyoko katika nafasi ya tatu na pointi zake 46 ingawa imecheza mechi tatu pungufu ya Azam yenye pointi 51.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limemtaja mwamuzi, Ahmed Arajiga kutoka Manyara atakuwa mwamuzi wa kati na atasaidiwa na Mohammed Mkono wa Tanga, Kassim Mpanga (Dar es Salaam) na Tatu Malogo (Tanga).

Akizungumza jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema hii ni mechi kubwa sana Afrika Mashariki na leo itakuwa ni sehemu ya



Djgui Diarra

Ayoub Lakred

INAENDELEA UK. 23

# Dabi 6 zisizosahaulika

**Na Adam Fungamwango**

MASHABIKI wa soka ndani na nje ya Tanzania wanatarajia kusimama kwa dakika 90 ili kushuhudia mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ni mchezo ambao unaongeza idadi ya mechi za watani wa jadi, yenye majina mengi, wengine wakiita Dabi ya Kariakoo, lakini kama kawaida, huingizwa katika vitabu vya kumbukumbu za soka na kusomwa na vizazi hadi vizazi pale watakapohitaji kupekua rekodi zake.

Rasmi rekodi za timu hizi zilianza kuwekwa mwaka 1968, ambapo pamoja na mechi nyingi kuchezwa, lakini kuna michezo kadhaa imebaki katika kumbukumbu hadi leo kutokana na matokeo yake ya kushangaza, vipigo vikubwa na kuweka rekodi ambazo hazijavunjwa.

Hizi ni baadhi ya mechi ambazo hadi leo zimebaki ni simulizi katika mechi za dabi.

**1. Yanga 5-0 Simba (1968)**

Mechi hii imeingia katika rekodi ya kuwa ni ya kwanza timu hizo kufungana mabao mengi katika mechi za dabi. Hii ilikuwa ni Juni Mosi, mwaka 1968. Yanga ikiiadhibu Simba mabao 5-0, ambayo yalifungwa na Maulidi Dilunga (mawili), Kitwana Manara (mawili) na Salehe Zimbwe alifunga bao moja.

**2. Simba 6-0 Yanga (1977)**

Simba ililipa kisasi cha kufungwa mabao 5-0 miaka tisa baadaye, ilipoikandika Yanga magoli 6-0, mechi ambayo hadi leo inashika rekodi ya timu kufungwa mabao mengi zaidi katika dabi.

Ni mechi ambayo pia imeweka rekodi ambao haijavunjwa kwa mshambuliaji wake, Abdallah Kibadeni ‚King' kufunga hat-trick'.

Mechi ilichezwa Julai 19, mwaka 1977, na mbali na King Kibadeni, mabao mengine mawili yalifung-

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >